# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## (KCSE PREDICTIONS 1-10)

***An Exclusive Top-Notch KCSE Model Prediction Questions.***

***A special preview of Possible Expected sample KCSE Questions Most likely to be Tested in the Forthcoming KNEC examinations.***

**SERIES 1**

***Proudly prepared by an Exceptional team of Experienced Veteran KNEC examiners within the National Group of Mwalimu Agency.***

*For Marking Schemes/Answers*

***0746 222 000***

**MWALIMU AGENCY**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 1 PAPER 1

**NAME…………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## MASWALI

1. **LAZIMA**
   Chamko la ugonjwa wa Korona lililemaza shughuli za michezo nchini. Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa na Waziri wa Michezo kubuni mikakati ya kufufua michezo katika taasisi za elimu nchini. Andika kumbukumbu za mkutano huo. **(alama 20)**

2. Vijana wamekuwa wakichelea kuhusika katika mchakato wa uchaguzi. Jadili vyanzo vya hali hii huku ukiwapendekezea vijana umuhimu wa kubadili msimamo huu. **(alama 20)**

3. Tunga Kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo: Achanikaye kwenye mpini hafi njaa. **(alama 20)**

4. Andika insha itakayomalizikia kwa:
   **...***nilipotua nchini, nilishusha pumzi, nikamshukuru Jalia kwa kuponea chupuchupu katika uvamizi huo.* **(alama 20)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 1 PAPER 2

**NAME…………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN………………………**

**DATE………………………………………**

### 1. UFAHAMU (Alama 15)

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.***

Kijiji cha Mulukoba kilikuwa na utulivu wa aina yake. Okolo alikuwa miongoni mwa wazaliwa wa eneo hilo. Katika miaka ya tisini alikuwa ameanza safari yake ya masomo katika Shule ya Msingi ya Magombe.Enzi hizo mshawasha na imani za watu zilihusu tu maswala ya elimu.

Okolo alifurahishwa na utangamano wa kijiji chao. Watu walishirikiana kazini, sherehe za arusi, matanga aghalabu shughuli ya mtu iligusa mwenzake. Anakumbuka vizuri ngoma zilizopigwa katika sherehe mbalimbali wanakikundi cha ‘Alaki’ wakiongoza ilikuwa burudani ya aina yake. Na je, baragumu lililopulizwa na Achwari kuwaita watu kununua nyama na kujuza watu kuwa fulani ameaga? Kwa kweli Mulukoba kilikuwa kijiji chenye ufanisi.

Kando na hayo, vyakula walivyokuwa navyo hasa samaki waliovuliwa mto Akanyo hususan kambare, walikuwa na ladha ya kupendeza. Okolo alifurahia sana samaki wa kukaushwa ‘kerewa’ namna wanakijiji walivyoita. Huyu alikuwa chaguo lake, mamake alipopika siku hiyo basi ukamilifu ulijaa moyoni mwake. Okolo alitumai kuwa atakapooa, basi mkewe ni sharti afahamu kuwa ‘kerewa’ ndicho chakula chake. Mto huu pia ulikuwa kitovu cha michezo ya kitoto, ulikuwa na vivukio vitatu, kwa Alaki, kwa Nikola na Bobobo. Kidimbwi kizuri cha kupiga binzi kilikuwa kivukio cha Nikola. Vivukio hivi viliitwa majina haya kutokana na mwenye ardhi palipo kivukio hicho. Mazingira ya pale pia yalimpendeza. Hili humfanya akumbuke hadithi aliyosoma chuo kikuu ya E. Kezilahabi kuhusu Mayai Waziri wa Maradhi wakiogelea mtoni. Enzi hizo za miaka ya tisini mwanzo mtu hakujisumbua na

lazima lazima za sabuni. Mradi umeona maji, kulikuwa na mawe ya kusugua mguu pale mtoni, wengine wangetumia mchanga nayo sabuni ilikuwa harita au matawi ya mti walioita 'sabuni ya wazee'. Yaani wakati huo binadamu alitumia mali asili kwenye shughuli zake za kila siku.Leo hii anapojitia marashi na hata mkewe kumkumbusha aina za sabuni nzuri, hucheka pasi yeyote kutambua kiini cha kicheko hicho.

Je, ukarimu nao wa wanakijiji. Enzi hizo watu walisaidiana. Anakumbuka babake akiwaalika wanakijiji katika sherehe tu za burudani. Atoka mchezo tiriri akiongoza burudani huku wengine wakila na kunywa. Bangaradesi mmoja wa wanakijiji angecheza wimbo wa Atoka kwa miondiko yote. Huo ndio ukamilifu uliokuwepo. Anakumbuka wagema wawili waliofahamika sana , Akong'o na Majimaji. Majimaji alikuwa rafiki wa dhati wa babake, kila mara babake angetaka kuonja kinywaji, Okolo angeshika njia hadi kwake. Pombe aliyoenzi sana babake ni 'chang'aa. Akongo alikuwa mmoja wa wagema wapenzi wa babake, alipotumwa kununua pombe, kila mara Akongo angempa kiasi kwenye gilasi kama mbinu ya kumkumbusha ukamilifu wa mwanamume Mulukoba kwani waliokosa kunywa pombe walionekana wanyonge katika jamii. Ukweli ni kuwa Okolo alionja pombe zote, hata zingine kubugia, lililompiga mshipa kila mara ni habari ingewafikia walimu wake, hilo tu lingempa kwaheri ya masomo.

Katika shughuli hizi zote, Okolo alishauriwa na mamake kutilia maanani masomo. Ni kutokana na hali hii ukaamua kupea masomoni kwa matumaini ya kuwa kuajiriwa na vilevile kufaa kijiji chake.

Ni miaka kumi na mitano baada ya Okolo kutimiza ndoto yake. Leo hii ni mkurugenzi wa matibabu katika mojawapo wa hospitali nchini. Hatua zake za mwanzo alizofanya ni kuenda kuwafaa wenzake na wanyonge kijijini, hususan wale waliosoma nao ambao hawakufaulu kielimu. Amefadhili wanafunzi wengi mayatima hadi shule ya upili. Ndoto yake ya kufaa kijiji chake, ule ustaarabu na ujamaa ndiyo- azma yake. Gari alilonunua angalabu humsaidia yeyote mwenye safari ya dharura au hata mgonjwa. Kwa kuwa anafanya kazi mjini, yeye hupenda kuwaletea wanawake kanga. Kwa kweli miaka mitano tu jina lake lilienea na kutawala Mulukoba na kuvuka mipaka zaidi. Japo babake ameaga, amewahi kuita kikundi cha wacheza ngoma cha 'Alaki' katika hafia ya kumkumbuka babake.
Kwa kweli, malezi aliyopata kwa misingi ya ujamaa ni tiyara inayompeperusha. Kila mara atokapo mjini, yeye husalimia angalabu kila jirani yake. Mapeni yakiwa mfukoni hakosi kumuani mwenye taabu. Lakini kwa sasa, Okolo ameanza kusadiki kisa alichosoma kwenye riwaya ya Said Ahmed ya utengano kuwa hakuwa kijichobadilika ila mabadiliko yenyewe. Okolo amejipata tu ni yeye anayegonga mlango ya watu kuwajulia hali. Hata majirani

waliofana kama yeye hawajali. Kutia msumari kwenye kidonda ni kuwa ukarimu wake umekuwa mada ya minong'ono kijijini.

Alipotangaza kuwania udiwani hakujua kuwa ilikuwa ni mbinu ya kuchunguza ufanisi wake. Juzi amepata habari kuwa kuna baadhi ya wanaodai kuwa yeye ni mwizi wa mali ya umma, wengine wanadai ana mazingaumbwe. Ajabu ni kuwa kuna wanaodai kuwa aila yake haijawahi kuwa na kiongozi hata mzee wa kijiji, hivyo basi hana nafasi pale. Kinachomkata maini zaidi ni kuna vidudu watu wanaopiga simu mjini kuchunguza kitovu cha hela zake. Lililomfikisha hatua ya leo ni kuwa amesikia kuwa kuna wale wanaomkejeli mamake kuwa muuza mboga tu atawezaje kuzaa kiongozi. Lo! Dunia ni hadaa, amesalimu amri!

## MASWALI

**(a)** Onyesha namna usasa na ukale umejitokeza kwenye kifungu hiki. **(alama 2)**

**(b)** Fafanua namna swala la kinyume limeendelezwa na mwandishi. **(alama 5)**

**(c)** Thibitisha kuwa jamii hii ina ustaarabu. **(alama 2)**

**(d)** Tambua matatizo manne katika jamii hii. **(alama 4)**

**e)** Eleza msamiati ufuatao kama uliyotumika katika kifungu. **(alama 2)**

I) kwaheri ya masomo. ……………………………………………..

II) amesalimu amri……………………………………………………

## 2. MUHTASARI: (alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Katika kipindi cha miaka iliyopita, kumekuwa na mfumko wa bei ya bidhaa muhimu hivi kwamba idadi kubwa ya raia wanalala njaa. Uchunguzi uliofanywa na mashirika ya kijamii kuhusu bei ya bidhaa hizo umeonyesha kuwa familia za kawaida zinatumia nusu ya mapato yao kununua chakula. Bila shaka yoyote, hili ni janga linaloendelea kutokota. Tunafahamu kuwa kupanda kwa bei ya petroli kimataifa kumechangia kuongezeka kwa bei hiyo ya vyakula, kwa namna moja au nyingine.

Mbali na vyakula, gharama ya kupanga nyumba, maji, stima na mafuta imepanda kwa muda wa miezi mitatu iliyopita kati ya Desemba na Januari 2017. Kwa mujibu wa Benki ya duniailiyozinduliwa hivi majuzi, kupanda kwa bei ya vyakula kumesukuma familia nyingi katika lindi la umaskini.

Ingawa serikali haina uwezo wa kudhibiti baadhi ya sababu zinazochochea kuongezeka kwa bei ya chakula nchini, haipaswi kutulia tuli ikisubiri suluhisho litokee kisadfa. Inasikitisha kwamba viongozi wetu wanatumia muda mwingi kuchapa siasa huku raia wa kawaida wakiendelea kuumia. Iweje basi katika vikao vyao vya hadhara wanasiasa wanatumia muda mwingi kuzungumzia maswala ya kugawanya wananchi na kufichua njama za kuwaangamiza wapinzani wao badala ya kueleza namna

watakavyokabiliana na janga lililopo la njaa. Ni lini watafahamu kwamba hauwezi kumtawala mtu mwenye njaa?

Kwa muda mrefu, baa la njaa limekuwa likihusishwa na maeneo ya kaskazini mwa nchi yetu; lakini kama uchunguzi ulivyoonyesha, familia nyingi nchini zinaumia na wengi hawawezi kumudu bei ya bidhaa muhimu kama sukari, unga, mafuta ya kupikia na kadhalika.

Wakati umewadia kwa serikali kuchukua hatua madhubuti kwa kuwa kama ilivyo ni vigumu kumtawala mtu aliye na tumbo tupu na ambaye hajijui wala hajitambui kuhusu atakapopata lishe.

**(a)** Ukizingatia taarifa uliyosoma, fafanua athari za mfumko wa bei kwa wananchi. *(maneno 35 - 40)* *(Alama 6 1 mtiririko)* **(alama 6)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

(b) Eleza mambo muhimu anayoyazungumzia mwandishi katika aya za mwisho nne. *(maneno 60-65)* *(Alama 8, 1 mtiririko)* **(alama 9)**

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## 3. SARUFI

**A.** Andika neno lenye kikwamizo sighuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya chini kati. **(al. 2)**

**B.** Bainisha uamilifu wa viambishi katika neno lifuatalo **(al 2)**

Viliwavyo

**C.** Eleza muundo wa silabi katika neno mbilikimo. **(al 2)**

**D.** Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu, kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo. **(al 2)**

**E.** Kanusha sentensi ifuatayo katika wingi **(al 2)**

Mwanafunzi huyo akisoma kwa bidii atapita

**F.** Ainisha vihusishi katika sentensi zifuatazo **(al 2 )**

**a)** Tunu ni mrembo kama mama yake

**b)** Watawasili kufikia juma lijalo

G. Tambua virai katika sentensi **(al 2 )**

Wenye bidii kazini wamesifiwa sana bungeni

H. Tunga sentensi sahihi ukitumia kiunganishi cha kulinganisha **(al 2 )**

I. Andika katika usemi wa taarifa **(al 2 )**

“Wanasiasa hawa wenu wakipigana hivi wataharibu nchi” Rais alisema

J. Changanua sentensi kwa jedwali **(al 4 )**

Jirani aliyenisaidia juzi ataondoka mwaka ujao.

K. Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo **(al 3 )**

Alawi alifumiwa mkeka mzuri na shangaziye kwa miyaa

L. Tambua aina za vishazi katika sentensi **(al 2)**

Lazima nile lishe bora ili niwe mwenye afya

M. Ainisha sentensi ifuatayo ukitumia vigezo viwili vikuu. **(al 2)**

Wanafunzi walikuwa wakiamka mapema

N. Bainisha maana mbili za sentensi ifuatayo **(al 2 )**

Mapunda alisema kuwa mkewe amesafiri

O. Andika sentensi ifuatayo katika wingi **(al 1 )**

Onyesha kivumishi katika sentensi ifuatayo

P. Geuza sentensi zifuatazo katika nyakati na hali katika mabano **(al 2 )**

**i)** Wanafunzi wanafanya mtihani ( ujao hali timilifu)

**ii)** Mtoto amekunywa maziwa (uliopita hali ya kuendelea)

Q. Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha miundo miwili ya ngeli ya U-ZI **(al 2 )**

R. Tunga sentensi sahihi yenye kitenzi halisi **(al 1 )**

S. Andika sentensi upya kulingana na maagizo **(al 2 )**

(i) Miti ilikatwa Nairobi ( tumia viwakilishi vya maneno yaliyopigiwa msitari

(ii) Mtoto amekula wali ( geuza katika kauli ya kutendwa)

T. Onyesha matumizi ya KI katika sentensi hizi **(al 2 )**

**(i)** Hakijapikiwa

(ii) Alinunua kimeza hafifu

## 4. ISIMUJAMII

MTU 1: Una shida gani?

MTU 2: Kichwa chaniwanga, tumbo lanisokota na ninahisi uchovu mwingi. Nisaidie tafadhali.

MTU 1: Pole, afya yako itakuwa shwari. Hizi tembe hapa zitakusaidia kupunguza maumivu. Unapaswa kuzitumia mara tatu kwa siku…

**(a) (i)** Tambua sajili hii **( alama 2)**

**(ii)** Kwa kutolea mfano, andika sifa tatu ambazo zingetumika katika sajili hii **( alama 3)**

**(b)** Umepewa jukumu la kuendesha shughuli ya mazishi kijijini mwako. Fafanua sifa tano za lugha utakayotumia wewe na waombolezaji wengine. **(alama 5)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 1 PAPER 3

NAME…………………………………………………. INDEX NO…………………

SCHOOL……………………………………….   SIGN………………………..

DATE……………………………………..

1. **LAZIMA**

**USHAIRI**

Wafungwa wa kila mahali
Niarifu zenu idhilali
Maombolezo na machofu mlokabili

Wavuvi wa kila bahari
Leteni nyavu zilokumba hatari
Na nguvu za mawimbi mlohimili

Mafalahi wa kila jimbo duniani
Nileteeni yenu matambara leteni
Leteni hiyo mikono majuruhi
Na yalonyauka matiti
Na kucha zenu maiti
Nyote leteni kwangu
Leteni haraka leteni

Naunda mikitaba yakini
Ya dhiki za maskini
Kumpelekea Manani
Ishapotiwa saini
na midomo ya wala njaa
lakini, enyi mafukara wa dunia

Hofu yangu kubwa namwambia
Mungu huenda ikatukia
Hajui kusoma ... hili nachelea

## MASWALI

**(a)** Ainisha shairi hili. Toa sababu ya jibu lako. **(alama 2)**
**(b)** Tetea kwa kutoa hoja **nne** kauli kuwa utungo huu ni ushairi**.** **(alama 4)**
**(c)** Idhini ya mshairi inajitokeza vipi? **(alama 3)**
**(d)** Eleza ujumbe uliofumbatwa katika utungo huu**.** **(alama 3)**
**(e)** Ukitolea mifano, onyesha mbinu inayotawala katika shairi hili**.** **(alama 2)**
**(f)** Ubeti wa mwisho unakatisha tamaa. Thibitisha. **(alama 3)**
**(g)** Eleza muundo wa ubeti wa kwanza na wa pili. **(alama 3)**

## RIWAYA: CHOZI LA HERI - ASSUMPTA MATEI

***Jibu swali la pili au la tatu***

**2** a) … haya imekuandama tangu usiku ukimtongoza fulani; siku za kuchora ramani ya Afrika kwa vyanda vya miguu, hadi sasa? Ama ni hizo mvi unaficha? Naskia ile *mid-life crisis* ikiwashika wazee ndiyo hivyo.

**i)** Weka dondoo hili kwenye muktadha wake. **(alama 4)**
**ii)** Tambua mbinu zozote tatu za kimtindo kwenye dondoo hii **(alama 3)**
**iii)** Jadili sifa zozote tano za msemewa **(alama 5)**

b) Thibitisha kauli kwamba **'kweli jaza ya hisani ni madhila'** kwa kurejelea wahusika **wanane** kwenye riwaya ya *Chozi la Heri*. **(alama 8)**

**3**. **Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha.** Thibitisha ukweli wa methali kwa kurejele maudhui yoyote kumi katika *Chozi la Heri* **(alama 20)**

## TAMTHILIA: KIGOGO - PAULINE KEA

***Jibu swali la nne au la tano***

**4.** "Alizaliwa na meno mdomoni. Kisirani huyu! Wataka kuniharibia siku yangu nile nini? Wafikiri nauza nyonga kama huyo Tunu wako?"
" ... Boza, tusikoseane heshima. Nita..."
"Jaribu uone! Ama unafikiri hao watu wenu, sijui watetezi wa nini watawatetea? Nanyi mheshimu uhuru wenu."

**a)** Bainisha vipengele sita vya kimtindo vilivyotumiwa kwenye dondoo. **(alama 6)**
**b)** Yatambue mandhari ambamo mazungumzo haya yanafanyika. **(alama 2)**
**c)** Onyesha jinsi mandhari uliyoyabainisha katika (b) yalivyotumiwa kuendeleza usimulizi wa hadithi. **(alama 12)**

**5.** "Jukumu la kulinda uhai. Kulinda haki. Kulinda uhuru… Hujasahau mafanikio…"

**a)** Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**
**b)** Fafanua hulka nne za msemewa zinazojitokeza ndani ya muktadha huu.**(alam 4)**
**c)** Onyesha msemaji alivyofanikiwa katika azma yake ukirejelea tamthilia zima. **(alama 4)**

## HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE

***Jibu swali la sita au la saba***

**6. Mame Bakari**

"Dunia we' dunia. Dunia ya mwenye nguvu, si ya mimi dhaifu wa nguvu. Dunia ya msumari moto juu ya donda bichi. Hao watu je?"

**i)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
**ii)** Fafanua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 4)**
**iii)** Thibitisha kauli "Dunia ya msumari moto juu ya donda bichi" ukirejelea **Hadithi ya Mame Bakari.** **(alama 6)**
**iv)** Fafanua jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika hadithi hii. **(alama 6)**

**7. Tulipokutana Tena**

Nadhani kicheko chake kiliwaambukiza wenzangu maana vicheko vya nguvu viliwapasuka pamoja. Kama unavyoona, hivi vilikuwa vicheko vya mzaha na utani. Miongoni mwetu sote, Kazu alicheka zaidi. Alicheka kicheko mpaka mbavu zikamtafuna. Na alipocheka basi, alicheka kwa namna ya ajabu iliyonifurahisha sana. Alicheka huku ameviringa ngumi mbele ya kinywa kama ambaye anazuia hicho kicheko chenye nguvu za kutoa ***mwangwi*** uliosafiri robo dunia. Isitoshe, alipocheka namna hiyo, alijirusharusha kitini na kujivuta nyuma kwenye mgongo wa kiti na kuinua miguu yake mpaka soli za viatu vyake zikaonekak. Kumtazama Kazu akicheka ni namna ya kituko. Kila siku nikiwa naye, mimi huhakikisha kwamba namchekesha kwa mzaha huu na ule ili nimwone namna anavyocheka. Hata hivyo, yeye naye hakuwa mchekeshaji mdogo.

"Aaa, hadithi za kichawi Kazu, ziko kila pahala duniani," nilimwambia kwa kujitetea. "Unakumbuka mkasa maarufu hapa penu wa chatu lililotambaa kutoka Mashariki hadi Magharibi huku limemeza maelfu ya watu tumboni? Lilisafiri kwa masafa ya zaidi ya kilomita mia tano hivi na kuwatema watu hao huko Magharibi!"

**(a)** Tambua mbinu tano za kimtindo katika dondo hili. **(alama 5)**
**(b)** Eleza jinsi mwandishi alivyofaulu kutumia mbinu rejeshi katika kuijenga hadithi ya Tulipokutana Tena. **(alama 5)**
**(c)** Onyesha umuhimu wa mandhari ukirejelea Club Pogopogo. **(alama 4)**
**(d)** Hakiki matatizo aliyoyapitia Bogoa Bakari aushini mwake. **(alama 6)**

## FASIHI SIMULIZI

**8.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata*.**

Mabibi na mabwana, ndugu na marafiki hamjambo! Nimefika hapa leo kushuhudia sherehe za vijana hao wanaofuzu kuingia utu uzimani. Tangu jadi mababu zetu waliandaa sherehe kama hizi ili kuwaandaa vijana wao kukabiliana na maisha ya usoni. Wanangu, utu uzima hautokani tu na viviga au kisu cha ngariba. Ni matendo na tabia. Naam, ni matendo na tabia. Katika jamii ya sasa watu humpima mtu kutokana na ufanifu wake kiuchumi, kielimu na kijamii. Mtu asiye na mali yake hubezwa kwa kutofanya bidii inavyostahili. Hivyo basi, nawashauri vijana wanaofuzu leo kuwa, mnafaa kutia bidii masomoni ili mustakabali wenu uwe mzuri. Katika nyakati zetu, ubingwa wetu ulipimwa katika fani ya vita na ngoma. Ungewasikia wanaume wakijisifu kwa wimbo wakisema:

*Ooh ooh ooh!*
*Mimi ni chuma inayoishi*
*Ningiapo vitani, macho yangu tu huwafisha wengi.*
*Viganja vyangu vimeiletea jamii yetu fahari*
*Wananiita Ngao.*
*Juzi ngomani niliwapiku wote*
*Wanawali waliniangukia kwa kutaka uchumba*
*Nani mwingine kama Ngao?*

Hata hivyo, hali katika jamii ya sasa ni tofauti. Ngoma imekuwa nyenzo ya burudani tu. Navyo vita vya kikabila vimepitwa na wakati. Wanaopigana aghalabu huchukiliwa hatua kali za kisheria. Elimu ni silaha ya pekee. Elimu itawafungulia milango ya heri. Ndugu na marafiki, nawaomba nyote muwasisitizie vijana hao umuhimu wa kuwatii walimu wao na kutia bidii masomoni watakaporudi shuleni. Msisite kuwaadhibu wanapokosea. Ni muhimu kukumbuka kuwa, mchelea mwana kulia hulia mwenyewe. Tulisimuliwa na bibi kuwa, hapo zamani za kale mwanamke fulani alificha mnyama hatari aliyekuwa akifukuzwa na mashujaa wa jamii. Baada ya mashujaa hao kuondoka, mnyama huyo alimla mwanamke huyo. Ingawa ni hadithi, kisa hicho kinatufunzwa kuwa, hatufai kuficha matendo mabaya ya wanetu. Tuwarekebishe mapema.

Nikimaliza naomba kuwajuza vijana hawa kuwa, tohara siyo ufunguo wa ulevi. Inahuzunisha kuwakuta vijana wadogo wamelala matopeni kwa kushindwa kutembea kutokana na ulevi. Wengine hubaki pale hadi asubuhi wakitumbuizwa na milio ya vyura. Nina matumaini kuwa, kundi hili litakuwa tofauti. Asanteni kwa kunisikiliza.

## MASWALI

**(i)** Tambua kipera katika dondoo. **(alama 1)**

**(ii)** Eleza sifa za kipera ulichotaja katika (i) **(alama 4)**

**(iii)** Eleza dhima zozote mbili za kipera ulichotaja katika (i) **(alama 2)**

**(iv)** Tanzu za fasihi huingiliana na kutegemeana. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu hiki. **(alama 5)**

**(v)** Eleza toni iliyobainika katika kifungu. **(alama 2)**

**(vi)** Fafanua mbinu za kimtindo zinazodhihirika katika kifungu hiki. **(alama 6)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 2 PAPER 1

**NAME…………………………………………………. INDEX NO.…………………**

**SCHOOL……………………………………….. SIGN.…………………………**

**DATE……………………………………..**

## MASWALI

**LAZIMA**

1. Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Elimu imeanzisha mfumo mpya wa elimu ya Umilisi. Mwandikie mhariri wa gazeti la Darubini ukitoa maoni yako kuhusu changamoto zinazotokana na mfumo huu. **(alama 20)**

2. Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili **(alama 20)**

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.
   ``Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe'' **(alama 20)**

4. Anza kwa kifungu kifuatacho.
   **......**Hapo ndipo iliponibainikia kuwa nilikuwa nikiogelea baharini pekee kinyume na wenzangu wote. **(alama 20)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 2 PAPER 2

**NAME…………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL…………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

**1. UFAHAMU: (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia***

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. <u>Inakera</u> zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi,

aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea had kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengi hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21, asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa <u>majukumu</u> mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyishwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo nakuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale hushia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine hushia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali 'mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

## MASWALI

**a)** Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**
**b)** Eleza dhana ya mwanamkiwa kwa mujibu wa kifungu. **(alama 2)**
**c)** Eleza imani za kijadi kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 2)**
**d)** Jadili masaibu yanayowakumba wanawakiwa. **(alama 4)**
**e)** Eleza haki mbili za kikatiba zilizokiukwa kuhusiana na wanawakiwa. **(alama 4)**
**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na kifungu. **(alama 2)**

**i)** Inakera
**ii)** Majukumu

## 2. UFUPISHO: (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii. Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

**a)** Fupisha aya tatu za kwanza za *(maneno 70 – 75)* *(alama 7, 2 za utiririko)*
Matayarisho
Jibu

**b)** Eleza udhaifu wa runinga na video. (*maneno 50 – 51)* *(alama 5, 1 ya utiririko)*
Matayarisho
Jibu

**3. <u>MATUMIZI YA LUGHA:</u>** **(alama 40)**

**a)** Taja aina mbili kuu za ala za kutamkia sauti **(alama 2)**

**b)** Taja mfano mmoja mmoja wa sauti zifuatazo **(alama 2)**
Kimadende________________________________________________
Kipasuo kwamizo____________________________________________

**c)** Huku ukitoa mfano, eleza maana ya sentensi sahili **(alama 2)**

**d)** Ainisha mofimu katika neno lifuatalo **(alama 3)**
Tulimpikia________________________________________________

**e)** Ainisha vitenzi katika sentensi: Kitabu anachotaka kusoma ki mezani **(alama 3)**

**f)** Tunga sentensi moja ukitumia kiunganishi kiteuzi **(alama 2)**

**g)** Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani? **(alama 2)**
a) Uzi____________________________
b) Muda__________________________

**h)** Tumia 'o' rejeshi ya kati katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Watu ambao walifika jana ni wale ambao walitoka mbali

**i)** Onyesha shamirisho kipozi na ala katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Mwindaji haramu alimuua ndovu kwa bunduki

**j)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 3)**
Kilipikwa jana jioni

**k)** Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi **(alama 2)**
Msingesoma kwa bidii, msingepita

**l)** Tunga sentensi moja kudhihirisha dhamira/jukumu hili **(alama 2)**
Rai/ombi

**m)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**
Mtoto ambaye alianguka jana ana maumivu mengi

**n)** Onyesha matumizi yoyote mawili ya kiwakifishi: koma/kituo **(alama 2)**

**o)** Tumia neno 'Nairobi' kama **(alama 2)**
Nomino
Kielezi

**p)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya kuku na gugu **(alama 2)**

**q)** Onyesha matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi **(alama 2)**
Mwongeleaji stadi anajishaua sana.

**r)** Andika katika usemi wa taarifa **(alama 2)**
"Wageni wangu watafika saa ngapi? Mama aliuliza

**s)** Unda nomino kutokana na kitenzi **(alama 1)**
Safari

## 4. ISIMUJAMII: **(alama 10)**

Nipe chai, andazi mbili na egg moja…………

a) Taja sajili inayorejelewa na maneno haya **(alama 2)**

b) Fafanua sifa nne zinazohusishwa na sajili hiyo **(alama 8)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 2 PAPER 3

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1. LAZIMA** **Alama 20**

**(a)** Taja hatua tano za kufanya utafiti **(alama 5)**

**(b)** Eleza kwa hoja tano, umuhimu wa kushiriki kama njia ya kukusanya data **(alama 5)**

**(c)** Kikundi cha Tamasha Bora kiliwasilisha maigizo katika ukumbi wa shule yenu. Fafanua kwa hoja tano sababu za uwasilishi wao kufanikiwa. **(alama 5)**

**(d)** Eleza msamiati ufuatao **(alama 5)**

(i) ulumbi
(ii) mbazi
(iii) lakabu
(iv) matambiko
(v) rara nafsi

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**KIGOGO PAULINE KEA**

*Jibu swali la 2 au la 3*

***2.*** 'Wewe ni popo: Kwa ndege hupo na kwa wanyama hupo.'

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. **(al 4)**
b. Taja na ueleze tamathali za usemi katika dondoo hili. **(al 4)**
c. Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya**.** **(al 6)**
d. Huku ukitoa mifano sita mwafaka, fafanua maudhui ya usaliti kama yalivyojitokeza katika tamthilia hii. **(al 6)**

**Au**

**3.** a. Kwa kutolea hoja kumi, onyesha matumizi ya kinaya ili kufanikisha maudhui mbalimbali katika tamthilia ya Kigogo . **(al 10)**

**b.** Jumuiya ya Sagamoyo inakumbwa na udhalimu chungu nzima. Thibitisha kwa hoja kumi. **(al 10)**

## SEHEMU C: RIWAYA

**ASSUMPTA MATEI: *CHOZI LA HERI***

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4.** Eleza ufaafu wa anwani “Chozi la Heri” **(al20)**

**AU**

**5.** “Kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika”

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(Alama 4)**

**b)** Eleza tamathali ya usemi inayoojitokeza katika dondoo hili. **(alama.2)**

**c)** Msiba huandamwa na msiba mwingine. Thibitisha kauli hii ukirejelea msemaji wa maneno kwenye dondoo **(alama 4)**

**d)** Eleza jinsi haki za watoto zimekiukwa katika riwaya ya Chozi la Heri. **(alama 10)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**Chokocho na Kayanda (Wah) *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine***

*Jibu swali la 6 au la 7*

***Tulipokutana Tena***

**6.** Ingawa mimi nilikuwa kitoto cha miaka mitano, nilihisi siku ile ilikuwa mbaya kwangu.

**(a)** Fafanua muktadha wa dondoo hili**.** **(alama 4)**

**(b)** Eleza toni ya dondoo hili. (**alama 2)**

**(c)** Eleza sifa sita za mzungumzaji wa kauli hii**.** **(alama 6)**

**(d)** Fafanua umuhimu wa usimulizi wa mzungumzaji katika kuijenga hadithi ya Tulipokutana Tena. **(alama 8)**

**Au**

7. Huku ukirejelea hadithi ya **Tumbo lisiloshiba** na **Shibe inatumaliza**, Fafanua madhui yaliyoonyeshwa kwenye mabano;

**Tumbo lisiloshiba** ( ukiukaji wa haki.) **(alama 10)**

**Shibe inatumaliza (**ubadhirifu**)** (alama 10)

## SEHEMU E: USHAIRI

**8.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wenginea watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakizifuata nyago
Hadi kwenye wako au, pasipo hata kupesa, walakukupa kisogo
Mtu kuwa tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Pindi kinunua kitu, hafurahi shaitani, bali tajawa chukizo
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwato ako tekelezo
Tamko lake ‘subutu’, kuondoa tumaini, na kukuliza wazo
Mtu kuwa tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui
Hana faida nyumbani, ni mtu akichimbaye, mradi usitumai
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Kwa hakika ni baka, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo
Bahati ina hadaa, kukupa alo sodawi, aibarili rowoyo
Mipangayo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaniyo
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa
Ningetoa azinio, lakini uwezo sina, kwa mazito kuambiwa
Ama nitimue mbio, fuadinininanena, akilini nazuiwa
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

## MASWALI

**a)** Jadili dhamira ya shairi hili. **(Alama 1)**
**b)** Eleza sababu za mtungaji kulalamika katika shairi hili. **(Alama 3)**
**c)** Eleza umbo la shairi hili. **(Alama 4)**
**d)** Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari/ tutumbi. **(Alama 4)**

**e)** Taja na utoe mifano ya aina nne za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi hili **(Alama 4)**

**f)** Toa mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi katika shairi hili . **(Alamfa 2)**

**g)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. **(Alama 2)**

**i)** Zani

**ii)** Faraghani

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 3 PAPER 1

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL……………………………………… SIGN…………………………**

**DATE……………………………………**

## MASWALI

### LAZIMA

**1)** Wewe ni chifu wa Kata ya Mwangaza. Umeandaa mkutano wa wanakata wako. Andika hotuba utakayo toa kuhusu mambo yanayoathiri utangamano wa kitaifa na hatua zinazoweza kuchukuliwa.

**2)** Fafanua hatua ambazo zimechukuliwa nchini ili kukabiliana na tatizo la unyanyasaji wa jinsia ya kike.

**3)** Andika insha itakayo dhihirisha maana ya methali hii.

***Ukicheza ujanani utalipa uzeeni***

**4)** Andika kisa kitakacho malizikia kwa maneno yafuatayo.

**...**sasa ninaelewa maneno yake kuhusu kufanya maamuzi ya busara. Sasa nimepata baraka za wazazi na ridhaa yakuishi pamoja.

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 3 PAPER 2

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN………………………**

**DATE………………………………………**

**1. UFAHAMU: (ALAMA 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*:**

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sababu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

## MASWALI

**a)** Yape makala haya kichwa. **(alama 2)**

**b)** Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. **(alama3)**

**c)** Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. **(alama 4)**

**d)** Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. **(al 2)**

**e)** Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. **(alama 3)**

**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. **(alama 1)**

Gandwa

## UFUPISHO: (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasiliano kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundishia. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkemu kwa mtu wa kila rika. Halikadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji wa stadi ya kujifundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu, huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemchemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo ya vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu huwa ni liwazo kutokana na shinikizo na migogoro tunayokabiliana nayo kila siku. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu. Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga huwa ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya wa kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia, kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanaowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa familia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii.

Ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa ya kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalani, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, na kadhalika. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya dawa za kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaotumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya wawaelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

**a)** Fupisha aya **tatu** za kwanza kwa maneno 70 – 75 *(alama 8, 1 ya utiririko)*

**Matayarisho**

**Jibu**

**b)** Eleza udhaifu wa runinga na video. (*maneno 50 – 51)* *(alama 5, 1 ya utiririko)*

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3.<u>MATUMIZI YA LUGHA</u> (ALAMA 40)

**a)** Eleza maana ya kipashio kidogo cha lugha. **(alama 1)**

**b)** Andika maneno yenye sifa zifuatazo: **(alama 2)**

i) kikwaruzo ghuna cha ufizi, vokali ya chini-wastani, kizuiwa ghuna cha midomo, kiyeyusho cha midomo, irabu ya chini-kati

ii) Kipua ghuna cha ufizi, kipasuo cha ufizi, irabua ya mbele-juu, nazali ghuna ya midomo, irabu ya nyuma-juu.

c) Ainisha uamilifu wa kisarufi wa mofimu kwenye neno hili. **(alama 3)**

Lilimjisha

**d)** Tunga sentensi **moja** kuonyesha matumizi **mawili** ya **"tu".** **(alama 2)**

**e)** Unda kitenzi kutokana na nomino **toba** kisha ukitungie sentensi. **(alama 2)**

**f)** Yakinisha kwa kutumia kiambishi cha masharti ya uwezekano kwa wingi. **(alama 2)**
Usiposoma kwa bidii hutofaidika.

**g)** Tumia nomino ya ngeli ya mahali dhahiri pamoja na kivumishi kirejeshi cha kati kwa sentensi. **(alama 2)**

**h)** Andika kinyume cha sentensi hii. **(alama 2)**
Mjomba alimtwika mwanawe mzigo akabana mlango.

**i)** Bainisha kijalizo katika sentensi ifuatayo. **(alama 1)**
Tajiri huyo shupavu ana magari makubwa mno.

**j)** Tunga sentensi kwa kutumia chagizo cha ulinganisho. **(alama 2)**

**k)** Andika upya sentensi kwa wakati uliopita hali endelevu, kauli ya tendesheka. **(alama 2)**
Wenyeji wamewapokea wageni kwa taadhima.

**l)** Tunga sentensi **moja** kuonyesha maana mbili za neno **tema**. **(alama 2)**

**m)** Ainisha aina ifuatayo ya sentensi kiutendakazi. **(alama 1)**
Safari imekuwa ikitusumbua sana.

**n)** Onyesha kiima na utambue muundo wake katika utungo huu. **(alama 2)**
Pesa zote zilihifadhiwa na mwekahazina shujaa.

**o)** Tumia kishazi tegemezi kwenye sentensi kuonyesha vigezo vifuatavyo. **(alama 2)**
i) Wakati
ii) Jinsi

**p)** Changanua kwa kielelezo cha mistari. **(alama 4)**
Aliponijia kwa mkopo, nilikuwa nasali sebuleni.

**q)** Andika upya kwa kuanza na yambwa tendwa. **(alama 2)**
Mvua iliwanyea wanunuzi sokoni hivi majuzi.

r) Tunga sentensi kwa hali ya kudunisha ukitumia kihusishi cha uhusiano. **(alama 2)**

s) Eleza matumizi ya kiambishi **po** katika sentensi. **(alama 2)**
Achezapo anapofika sisi hushangilia.

t) Twasema oyee tunapofurahia jambo………………………………..tunapotahadharisha na ……………….
Tunapotoa himizo. **(alama 2)**

## 4. ISIMU JAMII **(ALAMA 10)**

**a)** Eleza maana ya usanifishaji wa lugha. **(alama 2)**

**b)** Taja lahaja zozote mbili za kati. **(alama 2)**

**c)** Kulingana na habari zinazotufikia hivi punde, maafisa watatu wa polisi jana walikana mashtaka ya mshukiwa wa mauaji ya watoto 13 kutoroka kutoka kituo cha polisi.
i) Tambua sajili inayorejelewa. **(alama 1)**
ii) Eleza sifa **tano** za sajili hii. **(alama 5)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 3 PAPER 3

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

**SEHEMU A**

**USHAIRI**

1. ***Lazima***

**Monyara**

Nakumbuka kwa dhiki Mto Monyara
Tuliochelea kukaribia kingo zake
Tukatulia kwanza; ukakamavu kujihamia
Kwa kunyenyekea wingi wa yake maji
Yaliyojiendea utadhani yamesimama.

Ni katika mto huu
Ambapo samaki wakubwa tulivua
Maguo kuyatakasa japo kwa kunyemelea
Na walevi stadi wakachelea kuuvuka
Ulipofura na kupita kwa kiburi
Kwa kushiba maji yake
Yaliyofanya mawimbi madogo.

Ni hapa ambapo marehemu nyanya
Mkono alinishika na njia kuniongoza
Juu ya ulalalo wa miti
Vikapu vyetu hewani vikielea;
Mimi nikishika changu kwa mkono mmoja
Naye akikiachilia chake kujishikisha kichwani

Masafa baina yetu na mtambo
Uliokwenda kwa maji
Tuliyapunguza kwa kila hatua tulopiga.

Ni katika mto huu ambapo
Samaki tuliowavua tuliwapasua na kuwasafisha
Na hivyo kuuficha umaskini wetu
Ulotuzuia kununua mnofu wa bucha
Ni hapa ambapo wanawake walifika
Mawe ya kusagia kupata
Ni katika mto huu ambapo
Waumini walifika kutakaswa kwa ubatizo
Baada ya ulevi, uzinzi na kufuru nyinginezo.

Ni hapa ambapo ilisimuliwa kuwa
Hata wachawi walifika kufanya vitimbi vyao
Baada ya utawala wa jua kumezwa na nguvu za giza
Sasa Monyara nilioijua haipo tena
Zimebaki kingo zilizokaukiana
Kama uso wa mrembo aliyekosa mafuta
Siku ayami.

Mto huu ambapo pembeni mwake
Watoto walipashwa tohara
Maji yake yakishangilia, umekonda
Na mbavu zake nje kutoa
Na sasa vitoto vikembe vinazikanyaga
Vikijiendea zao kusaga mahindi
Juu mlimani
Katika mtambo wa Kizungu
Usioisha kulalamika
Nao wanawake hawaji tena
Kutafuta mawe ya kusagia wimbi
Imebaki njia ya walevi warejeao nyumbani
Nayo miti iliyosimama wima ukingoni
Iliisha kuanguka kwa kuleweshwa na pumzi za walevi
Wasioisha kupita hapa.

## MASWALI

**(a)** Onyesha umuhimu wa Mto Monyara kwa wanakijiji. **(alama 4)**
**(b)** Toa mifano ya mishata inavyojitokeza shairini. **(alama 2)**
**(c)** Eleza aina **tatu** za taswira zinazojitokeza katika shairi hili. **(alama 3)**
**(d)** Fafanua mtindo katika shairi hili. **(alama 3)**
**(e)** Tambua nafsi neni ya shairi hili. **(alama 1)**
**(f)** Jadili idhini ya kishairi katika shairi. **(alama 3)**
**(g)** Andika ubeti wa pili katika lugha nathari **(alama 2)**
**(h)** Eleza toni ya shairi hili. **(alama 2)**

## SEHEMU YA B

**Riwaya**: *Chozi la Heri* - Assumpta Matei

Jibu swali la *2 au 3*

**2.** "Wapo baadhi yetu ambao wizi unapotokea inasemekana wanashirikiana na wahalifu wenyewe na baadaye wanagawana ngawira nao!"

***a)***

**i)** Fafanua muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**
**ii)** Jadili mtindo katika dondoo hili **(alama 3)**
**iii)** Eleza sifa za usemaji wa dondoo hili **(alama 3)**

***b)*** Ufisadi unaojadiliwa katika dondoo una madhara katika jamii ya Wahafidhina. Jadili. **(alama 10)**

**3.**

*a)* ***Jadili mtindo kwenye dondoo hili.*** **(alama 8)**

Jua linalochomoza halina ule wekundu wa jua la matlai ambao huleta haiba ya uzawa wa siku yenye matumaini. Naona wingu kubwa angani likitembea kwa kedi na madaha na kulifunika jua. Tukio hili linafuatwa na umeme, kisha mtutumo wa radi. Mawingu yaliyoshiba yakataka kutapika yanagooka, yanakaribiana, kupigana busu na kusababisha mwanguko wa matone mazito ya mvua; matone yanayoanguka kwenye ngozi laini za wanangu wakembe, Lime na Mwanaheri. Nawatazama kwa imani lakini siwezi kuwasaidia. Sina hata tambara duni la kuwafunikia. Linalobaki ni kumshuru Mungu kuwa tungali hai. Ubavuni mwangu amelala maskini mke wangu,Subira. Sijui kama inahalisi kumwita mke wangu kwani huyu siye Subira wangu wa zamani. Siye, siye, siye-e-e-e. Tazama uso wake ulivyovamiwa na majeraha, kikwi. Tazama tambo lake lililoumbuka. Amevimba na kuvimbiana kama dongo la unga ngano baada ya kutiwa hamira. Lakini yeye hana la hamira! Haya ni matokeo ya ubahaimu wa binadamu. Kwa mbali namwona Ridhaa – mwamu hasa – akitafuna kitu fulani, nadhani ni mzizimwitu. Ridhaa, kweli Ridhaa kula mzizi! Daktari mzima! Mkurugenzi mzima wa Wakfu wa Matibabu nchini! Wanasema

wajuao kuwa simba akikosa nyama hula nyasi. Msafiri kafiri ati! Amekosa la maama, hili la mbwa ataliamwa!

***b)*** "Huyu hapa ni Bwana Mwangemi na huyu hapa ni Bi Neema. Kama nilivyokujuza hapo awali, wamekuja kuchukukua kwenda kuishi nao kama mwana wao."

- **i)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
- **ii)** Banaisha mtindo katika dondoo. **(alama 3)**
- **iii)** Toa sifa za msemaji wa dondoo hili. **(alama 5)**

## SEHEMU YA C

**Tamthilia:** *Kigogo* **-** Pauline Kea

*Jibu swali 4 au 5*

**4.** Mwandishi wa tamthilia ya *Kigogo* amefanikiwa katika kutumia ishara ili kufanikisha maudhui. **(alama 20)**

**5.** Mimi sili makombo kama kelbu! Nilishakunywa chai ya mke wangu nikaridhika."

(i) Eleza mkutadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(ii) Fafanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

(iii) Jadili vile Wanasagomoyo wamefanywa kelbu kula makombo **(alama 12)**

## SEHEMU D

**Hadithi Fupi:** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* - Chokocho Na D. Kayanda:

Jibu swali la *6* au *7*

**6.**

i) Tathmini umuhimu wa Samueli Matandiko Katika kuijenga hadithi, "Mtihani wa Maisha **(alama 10)**

ii) Fafanua shibe inavyomaliza Waafrika katika hadithi ya "Shibe Inatumaliza". **(alama 10)**

"Tulipokutana Tena" - Alifa Chokocho.

**7.** ***a)*** 'Jijini ni kuzuri. Kuna majumba makubwa, utapanda magari mazuri mazuri ya marafiki zetu, utakula vyakula vitamu na kupewa nguo za fahari. Utapelekwa shule kusoma na kwandika.'

- **i)** Jadili muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
- **ii)** Eleza taswira zinazojitokeza katika dondoo hili kwa kutoa mifano. **(alama 3)**
- **iii)** Aliyoambiwa msemewa ni kinyume cha yaliyotokea. Eleza. **(alama 8)**

**b)** Wahusika mbalimbali katika hadithi hii wanatumia njia nyingi kukabiliana na matatizo yanayowakumba. Zijadili **(alama 5)**

# SEHEMU YA E

## Fasihi Simulizi

Malaika …..
Nakupenda malaika x 2
Ningekuoa mali we…..
Ningekuoa dada…..
Nashindwa na mali sina we…..
Ningekuoa malaika x 2
Pesa, zasumbua roho yangu x 2
Nami nifanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina we
Ningekuoa malaika x 2

**i)** Tambua utungo huu. **(alama 2)**

**ii)** Toa sababu za jibu lako hapo juu **(alama 2)**

**iii)** Taja shughuli ya kijamii na shughuli ya kiuchumi inayodokezwa kwenye kipera hiki. **(alama 2)**

**iv)** Tambua nafsi neni na nafsi nenewa. **(alama 2)**

**v)** Jadili vipi mwasilishji wa kipera hiki anaweza kuboresha wasilisho lake**.(alama 6)**

**vi)** Ni matatizo yapi yanayoweza kumkumbuka mkusanyaji wa kipera hiki nyanjani? (alama 6)

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 4 PAPER 1

**NAME……………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## MASWALI

**LAZIMA**

1. Ukiwa waziri wa Elimu nchini, umealikwa kuwazungumzia wanafunzi wa Kidato cha nne katika shule ya Ufanisi. Andika tawasifu utakayowasilisha.

2. Wananchi ndio wakulaumiwa kutokana na kuzorota kwa usalama nchini Kenya. Jadili

3. Andika insha itakayoafikiana na methali
   Baniani mbaya kiatu chake dawa

4. Tunga kisa kinachomalizia maneno yafuatayo:
   **.....**Nilijitolea kafara na msaada wangu ukazaa natija kwa wengi.

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 4 PAPER 2

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## UFAHAMU: (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururu wa migomo na maandamano ya raia.Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama,kuku na ndege.La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti!

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo.Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu.Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunatajika muda mrefu ili kufaulu

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya.Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu.Swali ni je,hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya.Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru.

Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji.Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipya ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimimia maisha ya watu.Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

**Maswali**

**a)** Yape makala haya anwani mwafaka. (alama 1)
**b)** Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu. (alama 3)
**c)** "Ugatuzi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari" Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala (alama 3)
**d)** Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka serikali kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatuzi (alama 4)
**e)** Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu (alama2)
**f)** Eleza maana ya maneno yafuatayo (alama 2)
(i) Ugatuzi
(ii) Kibepari

**UFUPISHO (Alama 15)**

**Soma makala yafuatayo na ujibu maswali.**

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malghafi yanayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji, viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu hasa kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda. Katika msingi huu, viwanda vikubwa vitawiwa vigumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine.Uajiri huu wa wafanyakazi wengi ni

muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la uajiri ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasnia, mataifa yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapana, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hizo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa zenyewe.

Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo. Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa ni chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimesambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huu wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Licha ya faida zake, ueneaji au kutanda kwa viwanda hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Tatizo la kwanza linahusiana na mtaji. Lazima pawepo na mbinu nzuri za kuweka akiba ili kuwa na mtaji wa kuanzishia biashara. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kwa kutegemea masoko ya mitaji ambayo katika mataifa mengi hayajaendelezwa vyema. Inakuwa vigumu katika hali hii basi kupata pesa kwa uuzaji wa hisia kwenye masoko hayo.

Tatizo jingine linalotokana na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kibiashara kwa wenye viwanda vidogo vidogo. Mikopo ya aina hii huwa muhimu hasa pale ambapo anayehusika ana mradi wa kununua vifaa kama mashine. Mikopo ya muda mfupi inayopatikana kwenye mabenki huweza kuwashinda wengi kutokana na viwango vya riba kuwa juu. Haimkiniki kwa viwanda kama hivi kukopa kutoka nje ya nchi zao. Juhudi za kuendeleza viwanda hivi huweza pia kukwamizwa na tatizo la kawi kama vile umeme. Gharama za umeme huenda ziwe juu sana. Isitoshe, si maeneo yote ambayo yana umeme. Matatizo mengine huhusiana na ukosefu wa maarifa ya kibiashara, ukosefu wa stadi za ujasiriamali au kuwa na ujasiri wa kujiingiza kwenye shughuli Fulani na miundo duni.

Ili kuhakikisha kuwa viwanda vimekuzwa na kuendelezwa pana haja ya kuchukua hatua kadha. Kwanza, kuwepo na vihamasisho kwa wanaoanzisha viwanda vidogo vidogo kama vile punguzo la kodi, kuhimiza kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo na kusaka kuyapanua masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha kuanzishwa na kupanuliwa kwa taasisi za kuendeleza upanuzi huo. Pana haja ya kuwekeza kwenye rasilimali za kibinadamu; kuelimishwa na kupanua uwezo wao wa kuyaelewa mambo

mbalimbali. Miundo msingi haina budi nayo kupanuliwa na kuimarishwa.Upo umuhimu pia wa kuongeza kasima inayotengewa maendeleo na ukuzaji wa viwanda ili kuharakisha maendeleo yake pana umuhimu wa kupambana na ufisadi unaoweza kuwa kikwazo kikubwa. Inahalisi kutambua ikiwa viwanda vitatanda nchini, uchumi wa nchi nao utawanda.

**(a)** Kwa **maneno 65-75,** eleza ujumbe muhimu unaopatikana katika aya ya pili hadi ya nne. **( alama 8,1 utiririko)**

**Maandalizi**

**Jibu**

**(b)** Kwa **maneno (50-55)** fafanua mambo yanayotinga ukuaji wa viwanda. **(alama 5, 1 utirirko)**

Maandalizi

Jibu

## MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

**a)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa **(alama 2)**
Nyuso za vijana wale zilichujuka walipoanguka

**b)** Tumia **KI** katika sentensi kuonyesha masharti yanayowezekana **(alama 2)**

**c)** Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi **'abudu'** katika kauli ya kutendesheana **(alama 2)**

**d)** Akifisha **(alama 4)**
aisee yale mawimbi ya tsunami yaliyotokea bahari hindi yaliangamiza biashara nyingi sana alisema bomet

**e)** Changanua sentensi hii kwa njia ya mstari. **(alama 4)**
Rais alihutubu lakini walimpuuza

**f)** Huku ukitolea mfano eleza tofauti kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi **(alama 3)**

**g)** Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu lake **(alama 2)**
Pika ugali kwa kuku kila Jumamosi ukitumia gesi

**h)** Tunga sentensi moja ya kuonyesha rai **(alama 1)**

j) i Eleza maana ya chagizo **(alama 2)**

ii. Bainisha chagizo katika sentensi ifuatayo **(alama 1)**
Shamba lilipaliliwa haraka na mkulima

k).Andika katika usemi wa taarifa **(alama 3)**
"Hicho kijicho cha paka cheupe leo marufuku kwangu" alisema Mzee Kambumbu

l)Tunga sentensi moja ukitumia kitenzi kimoja kilichoundwa kutokana na nomino **zawadi** **(alama 2)**

m). Tambua matumizi ya kiambishi **ji** katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji yule

**n)** Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya neno: **ilmradi.** **(alama 2)**

**o)** Andika sentensi moja ukitumia kihisishi cha bezo **(alama 1)**

**p)** Ainisha viambishi katika neno **waliibiana** **(alama 2)**

**q)** Nini maana ya kiimbo? **(alama 1)**

**r)** (i) Vokali ni nini? **(alama 1)**

(ii) Eleza sifa mbili za sauti ifuatayo **/i/** **(alama 2)**

**s)** Panda ni kuatika mbegu ardhini au kuparaga mti. Andika maana nyingine mbili **(alama 2)**

## <u>ISIMU JAMII</u> (Alama 10)

**a.** Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la Kiswahili. **(alama6)**

**b.** Fafanua istilahi zifuatazo: **(alama 4)**

**i.** UwiliLugha

**ii.** LinguaFranka

**iii.** Misimu

**iv.** Sajili …

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 4 PAPER 3

**NAME…………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## SEHEMU A : TAMTHILIA

**Pauline Kea : Kigogo**

**1. LAZIMA**

**a)** Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

Yaani kusema kwamba mapenzi hayatiwi nyunguni na kutokoswa kama mahindi na maharagwe ni tusi tena? Ana nini kwani ambacho sina? Jamani mimi wa kulinganishwa na Samson Myahudi ama shujaa Lyongo wa waswahili. Nafikiri alikuzungusha ndonga. Mwambie uume si kuvaa suruali tu, hata wanawake wanazivaa.

**b) ...** hata wanawake wanazivaa. usemi huu unaafiki wahusika katika tamthilia, Jadili. **(alama 5)**

**c)** Msemaji wa maneno haya ni kigogo. Thibitisha **(alama 10)**

## SEHEMU B : RIWAYA, A. Matei : Chozi la Heri

*Jibu swali la 2 au la 3.*

**2.** a) ….. suala la usalama haliwezi tena kupuuzwa. Usalama ni mmojawapo ya mahitaji ya kibinadamu.

Thibitisha ukweli wa kauli hii. **(alama 10)**

b) Fafanua umuhimu wa mzungumzaji katika kujenga ploti. **(alama 10)**

**3.** 'Mimi sitakufa maskini'

a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

b) Eleza toni ya dondoo hili **(alama 2)**

c) Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai. Jadili. **(alama 14)**

## SEHEMU C: TUMBO LISILO SHIBA NA HADITHI NYINGINE.

**Wahariri: Alifa Chokocho na Damu Kayanda**

Jibu swali la 4 au la 5.

**4.** *Mohammed Khelef Ghassany* "Mame Bakari"

"……… Bwana na Bibi hawawezi kukuvunja,"

a) Eleza muktadha wa maneno haya. **(alama 3)**

b) Fafanua jinsi wazazi wa msemewa hawakumvunja. **(alama 7)**

c) Jadili 'mitihani' katika hadithi ya '*Mtihani wa maisha'* **(alama 10)**

**5.** Mtoto wa kiume amesawiriwa kupitia changamoto si haba katika jamii ya sasa.Tetea kauli hii ukirejelea hadithi ya *Ndoto ya Mashaka* , *Mapenzi kifaurongo* na *Masharti ya kisasa.* **(alama 20)**

## SEHEMU D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7.

**6.** ***Soma shairi lifuatalo kasha ujibu masuali***

**1.** Mkata ni mkatika, harithi hatorithiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa
Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa!
Mrithi nini wanangu?

**2.** Sina ngo'ombe sina mbuzi,sina kondesi na buwa
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa
Sinamazurimakuzi, jinsi nilivyoachiwa
Mrithi nini wanangu?

**3.** Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa
Sina chembe ya majazi, mno ni kukamuliwa
Nakwa'cheni upagazi, mgumu kwenu ku'tuwa
Mrithi nini wanangu?

**4.** Sina sikuacha jina, mkatahatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno ni kulaumiwa
Poleni wanangu sana, sina kwenu cha kutowa
Mrithi nini wanangu?

**5.** Sina leo sina jana, sina kesho kutwa liwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sana, la kwacha nakuraduwa

Mrithi nini wanangu?

6. Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ilidhiki, na mbele imekaliwa
N'na wana na mikiki, hadi n'tapofukiwa
Mrithi nini wanangu?

7. Sinai la kesho kwenu,wenyewe kuiongowa
Muwane kwanyingi,mbinu Mwende pasi kupuwa
Leo siyo, keshoyenu,kama mutaji kamuwa
Mrithi nini wanangu?

*(Kina cha maisha A.S.Mohammed)*

## MASWALI

**a)** Eleza hali ya mzungumzaji katika shairi hili **( alama 4)**
**b)** Eleza dhamira kuu ya mshairi kulitunga shairi hili **(alama 2)**
**c)** Ni nani anayezungumziwa na nafsi neni katika shairi hili? **(alama 2)**
**d)** Eleza toni ya shairi hili **(alama 2)**
**e)** Fafanua mbinu tatu za lugha zilizo tumiwa katika shairi hili **(alama 3)**
**f)** Tambua bahari ya shairi hili ukizingatia. **(alama 4)**
   a. Mizani
   b. Vina
**g)** Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya tutumbi **(alama 3)**

***8. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali***

Jama, Jama, Jamani
Mbona twabebeshwa mateso hivi
Mizigo mikubwa ya dhiki kama
Kwamba hatuna haki ya kusema
Kukataa ndoa za lazima
Kukataa kuozwa wazee
Kukataa kukatishwa masomo
Kukataa tohara ya lazima

Jama, Jama Jamani
Iweje tuteswe mateso haya
Na watu wasio kuwa hata na haya kama

Kwamba hatuna haki ya kulalamika
Kulalamikia kutumikishwa kama mayaya
Kulalamikia kudhalilishwa kiunyama
Kulalamikia kutolindwa na sheria

Jama, Jama, Jamani
Sasa hii ni awamu nyingine
Na macho tumeyafungua kabisa
Tumekataa kudhalilishwa kabisa
Tumekataa kuteswa kama watumwa
Tumekataa tohara ya lazima
Tumekataa kuozwa....... Tumekataa! Tumekataa
Hii awamu ya 'Haki ya mtoto wa kike'

## MASWALI

**a)** Hili ni shairi la aina gani? **(alama 1)**
**b)** Taja na ueleze mambo matatu muhimu yaliyozungumzwa na mshairi **(Alama 3)**
**c)** Eleza muundo wa shairi hili **(Alama 4)**
**d)** Taja mbinu mbili za lugha alizotumia mshairi kufanikisha shairi lake (**Alama 4)**
**e)** Kwa nini mshairi huyu anasema hii ni 'awamu' nyingine? (**Alama 3)**
**f)** Eleza matumizi ya mishata katika shairi hili **(alama 2)**
**g)** Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi **(alama 3)**

(i) awamu
(ii) kudhalilishwa
iii) Dhiki

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** **a)** Wewe ni mwigizaji wa michezo ya jukwaani. Eleza mambo sita ambayo utazingatia ili kufanikisha uigizaji wako. **(alama 6)**

b) Mbinu ya uigaji sauti ina umuhimu gani katika fasihi simulizi: **(alama 4)**

c) Soma utungo ufuatayo kisha ujibu maswali. **(alama 10)**

Mwananguuu , ni wewe kweli !
ndimi niliyekupa uhai mwana unoringia,
Anokufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu na waone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa
Laana wakumiminie,

Uje kuzaliwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakazamwanao wasikuuguze katika utu uzimawake
(kutoka – Fani ya Fasihi Simulizi)

## Maswali

**i)**Tambua kipera hiki cha Fasihi simulizi **(alama 1)**
**ii)**Eleza sifa zozote nne za kipera hiki cha Fasihi Simulizi **(alama 4)**
**iii)** Eleza kwa kutoa ithibati jinsia ya nafsineni? **(alama 1)**
**iv)**Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii**.** **(alama 4)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 5 PAPER 1

**NAME……………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL…………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## MASWALI

1. **LAZIMA**
   Unyakuzi wa ardhi umekuwa swala tata nchini katika siku za hivi majuzi. Andika tahariri ya gazeti la Mzalendo huku ukipendekeza suluhisho kwa tatizo hili.

2. Udanganyifu katika mitihani ya kitaifa umeleta madhara kwa wanafunzi. Eleza

3. Ng’ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini.

4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa:

**…………..**hapo ndipo nilipogundua kwamba Bahati alikuwa moto wa kuotea mbali.

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 5 PAPER 2

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

**1. UFAHAMU**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.***

Vipindi mbalimbali vya historia vimeshuhudia kuibuka kwa magonjwa ya ajabu. Magonjwa hayo yamehangaisha watu na kuzishughulisha bongo za wanasayansi na madaktari katika kutafuta tiba. Magonjwa kama vile tauni, kifua kikuu, homa ya matumbo na ndui ni baadhi ya yale yaliyotisha sana nyakati fulani za historia ya binadamu. Magonjwa haya yaliwaua maelfu ya watu na kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu.

Hata hivyo magonjwa hayo yaliweza kuchunguzwa na kutafutiwa tiba kabla ya kumaliza kabisa kizazi cha binadamu. Lakini hii ni baada ya kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. Ulimwengu wa sasa unashuhudia janga jingine la maradhi sugu ya Ukimwi. Neno "UKIMWI" lilitoholewa kutokana na athari za ugonjwa huo mwilini. Neno "UKIMWI" humaanisha Ukosefu wa Kinga Mwilini, ambapo herufi za kwanza za maneno matatu ziliunganishwa pamoja na kuunda neno hilo. Ugonjwa huu ambao tayari umewaua mamilioni ya watu kote ulimwenguni unazidi kuenea kwa kasi, mfano wa moto katika kichaka. Kutokana na kasi yake ya kuua watu, ugonjwa wa UKIMWI umepewa majina kama vile 'umeme' na pia 'ugonjwa wa vijana'. Watu wengi wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI ni wale walio na miaka kati ya 15 hadi 49. Kundi hili kwa kweli ndilo, linalohesabiwa kuwa na nguvu za kutunza jamii kwa njia nyingi. Iwapo wengi katika kundi hili watakumbwa na maradhi haya, watasalia wakongwe na watoto wasioweza kujimudu.

Nchini Kenya, UKIMWI uligunduliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1984. Kufika mwezi wa Juni 1996, inakisiwa kuwa ugonjwa huu ulikuwa umewaua watu wapatao 65,647 nchini . Hivi sasa, inasemekana kuwa takriban watu zaidi ya 500 hufa kila siku nchini Kenya kutokana na janga hili. Aidha, imethibitishwa kwamba takriban wafu milioni mbili u

nusu tayari watapoteza maisha yao kutokana na kuambukizwa virusi vya ugonjwa huu humu nchini. Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa.

Kutokana na kuongezeka kwa visa vya UKIMWI, hospitali na zahanati nyingi kote nchini zinashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa. Kwa hivyo makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwahudumia wagonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya makundi hayo hutoa tiba ya kisaikolojia pamoja na kuwapa ushauri wa hima ya kuishi, badala ya kukata tamaa. Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani kwao.

Lakini jambo la kuzingatia ni hili, tujifunze kutokana na historia. Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba ya ugonjwa huu itapatikana. Hii ni kwa sababu tumethibitishiwa haya kutoka katika historia yetu wenyewe. Ikiwa magonjwa yaliyosababisha vifo vya wengi kutokana na ukosefu wa tiba yalitokomezwa kupitia juhudi za kimatibabu, sembuse huu ugonjwa tulio nao sasa? Huku tukijikinga kutokana na maradhi haya tusife moyo bali tuwe na matumaini kwani subira huvuta heri.

## MASWALI

**a)** Fafanua maana ya vifungu vifuatavyo

**i)** Kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu. **(Alama 1)**

**ii)** Kuwasukuma maelfu ya watu kaburini**.** **(Alama 1)**

**b)** Eleza aina ya magonjwa yafuatayo:-

**i)** Homa ya matumbo **(Alama 1)**

**ii)** Kifua Kikuu **(Alama 1)**

**c)** Kwa nini ugonjwa wa UKIMWI umepewa majina ya kimajazi? **(Alama1)**

**d)** Eleza madhara yoyote matatu ya UKIMWI kulingana na taarifa **(Alama3)**

**e)** Ni harakati zipi zinazoendelezwa kukumbana na janga hili? **(Alama2)**

**f)** Eleza mienendo inayopaswa kuendelezwa kuondoa kukata tamaa **(Alama3)**

**g)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa.

**i)** Takriban……………………………………**……………………………** **(Alama 1)**

**ii)** Hima ya kuishi……………………………………………… **(Alama 1)**

## MUHTASARI

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umasikini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya Wakenya milioni 10 wamo hatarini ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia 75 ya Wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia kuiletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mazao ya mauzo katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa masuala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja. Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia 75 ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo.

Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo ya Kusini mwa Sahara umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya kiuchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umasikini.

Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kwa mfano, kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kuhifadhi kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo.

Bila hiyo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

## MASWALI

**a)** Kwa kutumia maneno kati ya 70-75 eleza ni kwa nini kuna haja ya serikali kutilia maanani na kuimarisha kilimo nchini (alama 6, 1 mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

**b)** Eleza namna serikali inavyoweza kumaliza njaa na umasikini nchini (maneno 60-70) (alama 9, 1 mtirirko)

**Matayarisho**

**Jibu**

## MATUMIZI LA LUGHA

**a)** Eleza kwa kutoa mifano tofauti kati ya ala tuli na ala sogezi. **(Alama2)**

**b)** Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo. **(Alama 3)**

- **i.** Nafsi ya tatu umoja
- **ii.** Wakati uliopita
- **iii.** 'O' Rejeshi
- **iv.** Kitendwa

v. Mzizi
vi. kiishio

**c)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali **(Alama 3)**
Mkoba ambao uliporwa umepatikana

**d)** Onyesha aina mbalimbali za nomino katika sentensi ifuatayo.
Kerubo amerudishiwa Jembe alilonyang'anywa. **(Alama 2)**

**e)** Andika sentensi yakinishi kutokana na ifuatayo **(Alama 1)**
Ng'ombe hajakamuliwa maziwa yote

**f)** Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii
Miti iliyokatwa na vibarua jana imebebwa leo asubuhi **(Alama 2)**

**g)** Kwa kutunga sentensi eleza matumizi mawili ya kistari kirefu **(Alama 2)**

**h)** Nyambua kitenzi cha silabi moja kifuatacho katika hali ya kutendea, kutendwa/tendewa na kutendeka na kutendeana
(Ku) cha **(Alama 2)**

**i)** Andika sentensi zifuatazo kwa Udogo.
Watu wale ni weusi tititi hawaonekani gizani **(Alama 2)**

**j)** Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi
Ruheni alishauriwa na kasisi aache tabia ya ulevi **(Alama 2)**

**k)** Tunga sentensi moja itakayodhihirisha maana ya maneno haya mawili
Shombo **(Alama 2)**
Chombo

**l)** Neno 'tikiti' hupatikana katika ngeli mbili tofaouti. Taja ngeli hizo na utunge sentensi kwa kila moja. **(Alama 4)**

**m)** Andika sentensi ifuatayo ukitoa kinyume cha maneno yaliyopigwa mstari
Kijana aliyekwea mlima ule alisifiwa sana **(Alama 3)**

**n)** Kanusha sentensi ifuatayo
Jamila akiimba vizuri atapewa zawadi **(Alama 2)**

**o)** Onyesha nomino zinazoweza kuundwa kutokana na vitenzi vifuatavyo **(Alama 2)**
i. Sarifu ...............................................................
ii. Sebeha ...............................................

**p)** Eleza maana mbili ya sentensi hii
Shamba letu limelimika **(Alama 2)**

**q)** Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo
Mume alimpikia chai mkewe kwa jiko **(Alama 3)**

## ISIMUJAMII

1. Taja na ufafanue nadharia tatu zinazoelezea asili ya lugha ya Kiswahili **(Alama 6)**

2. Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimujamii
   (a) Lafudhi **(Alama 2)**

   (b) Rejesta **(Alama 2)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 5 PAPER 3

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL……………………………………… SIGN…………………………**

**DATE……………………………………**

## 1.SEHEMU A: USHAIRI (LAZIMA)

Eti
Mimi niondoke hapa
Niondoke hapa kwangu
Nimesaki, licha ya risasi
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi
Siondoki
Siondoki siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Kwa mateke hata na mikuki
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa
Siondoki
Mimi ni Pahame!
Niondoke hapa kwangu!
Fujo na ghasia zikizuka
Na kani ya waporaji, siondoki

Haki
Siondoki
Kwangu siondoki

Niondoke hapa kwangu!
Nawaje; waje wanaokuja
Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe
Siondoki
Ng'oo hapa kwangu!
Katizame chini mti ule!
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi
Nende wapi?
Si hapa kitovu changu
Niondoke hapa kwangu
Wangawa na vijikaratasi
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu
Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii
Wala si makaratasi, siondoki

## MASWALI

**a)** Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini **(alama 2)**
**b)** Taja masaibu anayopitia mzungumzaji **(alama 4)**
**c)** Eleza toni ya shairi hili **(alama 2)**
**d)** Eleza muundo wa shairi hili **(alama 3)**
**e)** Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba **(alama 2)**
**f)** Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari **(alama 4)**
**g)** Tambua idhini moja ya mtunzi **(alama 1)**
**h)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi **(alama 3)**
(i) Karatasi
(ii) Nimesaki
(iii) kitovu

## 2.SEHEMU B TAMTHILIA YA KIGOGO

**2.**Uliona nini kwa huyo zebe wako ? Eti mapenzi!

**a.** Eleza muktadha wa dondoo. **(al. 4)**

**b.** Andika mbinu za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili **(al. 4)**

**c.** Taja hulka za mnenaji unajitokeza katika dondoo. **(al. 2)**

**d.** Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirekjelea tamthilia.**(10**

3.wa kurejelea tamthlia ya 'Kigogo ya Pauline Kea, onyesha jinsi ambavyo viongozi wengi katika nchi za kiafrika wamejawa na tamaa. **(alama 20)**

## SEHEMUC.RIWAYA YA CHOZI LA HERI(ASSUMPTA MATEI)

4.“ Kwa kweli ni hali ngumu hii”

Weka dondoo katika muktadha wake. **(alama4)**

Ni hali gani yamsemewa inayorejelewa kwenye dondoo. **(alama16)**

**5)** Ukabila ni tatizo sugu katika nchi nyingi za Kiafrika. Tetea kauli hii ukilejelea Chozi la Heri **( al. 20)**

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine**
**jibu swali la 6 au la 7**

6.Ukirejelea hadithi zifuatazo, eleza jinsi maudhui ya mapenzi na asasi ya ndoa yanavyojitokeza. **(alama20**

a) Mapenzi ya kifaurongo
b) Masharti ya kisasa
c) Ndoto ya Mashaka
d) Mtihani wa maisha

Au

**Shibe inatumaliza : Salma Omar Hamad**

7.“Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine ?”

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b)Eleza sifa za msemaji. **(alama 6)**

c) Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabadhirifu. **(alama 10)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8a)** Fafanua mchakato/fomula ya uwasilishaji wa vitendawili. **(alama4)**

b) Linganisha naulinganue vitendawili na methali. **(alama10)**

c) Toa sababu sita za kudidimia kwa fasihi simulizi. **(alama6)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 6 PAPER 1

**NAME…………………………………………………. INDEX NO…………………**

**SCHOOL…………………………………………    SIGN………………………**

**DATE…………………………………….**

## MASWALI

1. **LAZIMA**

   Andika mazungumzo kati ya Mwalimu mkuu na mzazi kuhusu chanzo, matumizi na athari za dawa za kulevya miongoni mwa vijana wengi wa siku hizi.

2. Hakuna kizuri kisichokosa ila. Thibitisha methali.

3. Fafanua hatua zozote zinazoweza kuchukuliwa ili kukabiliana na janga la umaskini hapa nchini.

4. Nilikuwa nimelala fo!fo!fo!nilipogutushwa na kishindo kikuu kutoka upande wa mjini**….**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 6 PAPER 2

NAME………………………………………………… INDEX NO…………………

SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………

DATE………………………………………

## 1. UFAHAMU (ALAMA 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa.***

Taifa la Kenya limekuwa na tatizo la njaa kwa muda mrefu na hili ni tatizo ambalo hutokea mwaka baada ya mwaka. Kuna sababu kadhaa ambazo zimelifanya tatizo hili likithiri. Wananchi wengi hutegema ukulima kujipatia pato pamoja na chakula. Jambo hili limekuwa shida kubwa kwa vile kilimo hutegemea mvua isiyotabirika. Watabiri wa hali ya hewa huwashauri wakulima wapande mbegu zitakazohimili jua lakini mvua nayo inakuwa nyingi na kuharibu mimea.

Bidhaa za ukulima kama mbegu za kupanda, mbolea, dawa za kunyunyizia na zinginezo, zimekuwa ghali. Kuna sehemu kubwa ya ardhi ambayo ni kame na haiwezi kutumika kwa kilimo. Mazao yanayotolewa shambani hayahifadhiwi vizuri. Mengine yanaharibikia shambani na mengine yanavamiwa na wadudu kiasi kwamba hayawezi kutumika.

Tatizo lingine ni vita vya kikabila. Kabila tofauti zinapopigana, watu huhama na kuacha mashamba ilhali wengine huchoma maghala ya chakula. Wafanyabiashara pamoja na serikali huwanunulia wakulima mazao yao kwa bei ya chini sana mpaka wanakosa shauku ya kuyashughulikia mashamba yao. Siku hizi wakulima hawashughuliki tena kuzuia mmomonyoko wa udongo. Hivyo mvua inaponyesha rotuba yote inachukuliwa. Serikali haina sera mwafaka za **kukabiliana** na njaa. Hii ndiyo sababu sehemu zingine kama Turkana na Marsabit zimekabiliwa na njaa kwa muda mrefu.

Tatizo hili linaweza kutatuliwa ikiwa wakulima wataelimishwa juu ya mbinu bora za ukulima. Pia wakulima waishio katika sehemu ambazo hazina mvua ya kutosha wapewe mbegu ambazo zitahimili kiangazi. Ukulima wa kunyunyuzia mimea maji unafaa kuzingatiwa. Mazao yanayotolewa shambani yahifadhiwe vizuri kwa kuwekwa dawa za

kuwaua wadudu.

Sehemu kubwa za ardhi ambazo hazitumiwi zitolewe kwa kilimo. Ni muhimu wakulima waelimishwe kuhusu jinsi ya kuzuia mmomonyoko wa udongo na umuhimu wake. Wakulima wanunuliwe mazao yao kwa bei nafuu ili wajibidiishe katika kazi yao. Serikali inafaa iwe na sera mwafaka ili iweze kutatua tatizo hilo ambalo limekuwa ni **janga** kuu.

## MASWALI

**a)** Eleza mbinu tano zinazoweza kutumiwa kutatua tatizo **kuu** linalozungumziwa. **(al 5)**

**b)** Fafanua matatizo mbalimbali yanayolikumba Taifa la Kenya. **( al 4)**

**c)** Onyesha ukulima ulivyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa la Kenya **(al 2)**

**d)** Vita vya kikabila husababisha njaa. Dhibitisha kwa mujibu wa kifungu. **( al 2)**

**e)** Eleza maana ya maneno haya kama yaliyotumika katika kifungu. **(al 2)**

i) Kukabiliana

ii) Janga

## 2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Sawia na inavyotumika katika kukuza uchumi, teknolojia haiwezi kuepukika katika malezi enzi hizi na zijazo. Watalaamu wa malezi dijitali wanasema ingawa wazazi wanafaa kuhakikisha watoto wao wanakingwa na hatari za mtandao, unaweza kutumiwa kukuza talanta zao.

Kulingana na mtaalamu wa malezi, wazazi wanaweza kutumia mitandao ya kijamii kukuza vipawa vya watoto wao huku wakihakikisha usalama wao. Watoto wanaweza kutumia mitandao kuandika blogu au kujifunza kupiga, kutangaza na kuuza picha na video. Wanaweza kunoa vipawa vyao katika michezo pia. Hivyo basi, wazazi wanapaswa kuwahimiza waingie katika mtandao na kuwa wabunifu.

Wataalamu wanasema wazazi wanaowaruhusu watoto wao kuanza kutalii mtandao kwa lengo la kukuza talanta zao huwa wanawapa ufunguo wa ufanisi wa maishani. Mtaalamu mmoja kwa jina Aluoch alieleza kuwa, kukumbatia mtandao ni njia moja ya mtoto wako kuweka rekodi ya ufanisi wake. Iwe ni picha wakipokea zawadi, wakishiriki na kushinda mechi au wakiwa kwenye hafla muhimu kwa maisha yao. Jambo hili linaweza kuwatia moyo kukuza talanta zinazoweza kuwafaa katika maisha yao ya baadaye.

Hata hivyo, wazazi wanafaa kuchunguza na kupitisha chochote watoto wao wanapakia au kuchapisha kwenye mtandao ili wasihatarishe maisha yao na ya familia zao. Ni muhimu kuwa makini ili watoto wasiandike maelezo au kuchapisha chochote kinachoeleza wanakoishi, wanakosemea au wanakoshinda wakicheza. Vitu vinazoweza kuepukwa ni kama sare za shule, picha zinazoonyesha nyumba yako au anwani ya nyumba au chapisho lolote linalotangaza watakakokuwa na wakati watakuwa hapo.

**MASWALI**

a) Fupisha aya tatu za kwanza. ( maneno 80-85). (alama 9, moja ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

b) Fupisha aya ya nne. (maneno 35-40) (alama 4, moja ya mtiririko)

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**a).** Andika sauti zanye sifa zifuatazo: **(al 2)**

i) Kipasuo, si ghuna cha ufizi

ii) Kikwamizo, ghuna cha ufizi

iii) Nazali, ghuna ya kaakaagumu

iv) Irabu ya mbele, juu, tandazwa

**b)** Tunga neno lenye sauti mwambatano ya ufizi. **(al 1)**

**c)** Kwa kutoa mifano, eleza tofauti ya silabi wazi na funge. **(al 2)**

**d)** Andika sentensi ifuatayo katika umoja. **(al 2)**

Tukipanda ndizi hizi vyema, vijiji hivi vitakuwa na vyakula vya kutosha.

**e)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao **(al 2)**

KN(W+V) + KT (t+ s)

**f)** Ainisha viambishi awali na tamati katika neno lifuatalo. **( al 2)**

Ulijuaje

**g)** Onyesha na kutoa mifano, miundo miwili ya nomino katika ngeli ya KI-VI. **( al 2)**

**h)** Yakinisha sentensi hii katika nafasi ya pili. **( al 1)**

Wasiposoma kwa bidii hawatapita mtihani.

**i)** Akifisha sentensi ifuatayo. **(al 3)**

tafadhali nipe maji ninywe nina kiu mkimbizi alimwambia

**j)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo umoja. **( al 1)**

Ngoma hizo zao zilipasuliwa na vijana wale.

**k)** **Tunga sentensi** moja ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendua. **( al 2)**

Funga

Chomeka

**l)** Unda vivumishi kutokana na vitenzi vifuatavyo kisha utunge sentensi ukitumia vivumishi ulivyotunga. ( al 2)

**i)** **Cheka**

Kivumishi…………………………………………………………………………

Sentensi…………………………………………………………………………

**ii)** **Pika**

Kivumishi…………………………………………………………………………

Sentensi…………………………………………………………………………

**m)** Tumia neno **hadi** katika sentensi kama kihusishi cha: **(al 2)**

i) wakati

ii) mahali

**n)** Tambua aina za vielezi katika sentensi ifuatayo: **(al 2)**

Kipusa mrembo sana alitembea kitausi shuleni jana.

**o)** Huba ni kwa penzi, heshima ni kwa …………………na ruhusa ni kwa **…….(al 1)**

p) Tambua aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo. **(al 2)**

Kijana aliyekuwa hapa ndiye mtoto wake.

**q)** Tambua shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. **(al 3)**

Vijana hawa hulipiwa karo mapema.

**r)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali. **(al 2)**

Zawadi nzuri niliyomtunuku mwanawe ilimpa furaha tele.

**s)** Tunga sentensi mbili ukitumia neno "komaa" kama: **(al 2)**

Kivumishi

Nomino

**t)** Ainisha virai katika sentensi ifuatayo; **(al 3)**

Ndovu amelala kando ya mti.

**u)** Tunga sentensi moja kudhihirisha maana tofauti za maneno; **Fuma** **(al 1)**

## 4. <u>ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>

**i)** Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ahabu: Likizo ilikuwa fupi tumerudi kwa vitabu sasa.

Munini: Huu ni wakati wa kipindi cha lala salama, lazima tujikaze.

Ahabu : Usemavyo ni real.

Munini: Bidii ndiyo itakayotuokoa.

Ahabu : Ulimaliza ile assignment. Maze mimi nilishindwa.

Munini: Shsss… ndo huyo mwalimu.

Bw. Juma: Nani hao wanaongea? Nyamazeni! Tumekuja hapa kusoma sio kupiga kelele.

## <u>MASWALI</u>

**a)** Tambua sajili inayorejelewa katika kifungu hiki. **(alama 1)**

**b)** Fafanua sifa nne za sajili hii kama zilivyojitokeza katika kifungu **( alama 4)**

**ii)** Taja nadharia tatu zinazoeleza chimbuko la lugha ya Kiswahili. **( alama 3)**

**iii)** Eleza istilahi zifuatazo katika isimu jamii **(alama 2)**

**a)** Usanifishaji

**b)** Lafudhi

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 6 PAPER 3

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## SEHEMU A: USHAIRI

**1. Lazima**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*.**

**KAMA SODOMA!**

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Haihitaji makini, kwa mwenye macho mazima
Utaona walakini, mradi ukitizama
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wanazini hadharani, wana kwa watu wazima
Wanatafuna maini, vijana na kina mama
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Hawana haya nyusoni, wameharamisha wema
Baba na binti ndani, wanacheza lelemama
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Marijali wa mbioni, kujipagaza umama

Wameikataa dini, toka tumboni mwa mama
Wadai Wataliani, watajirisha mapema
Yafanana na sodoma, mji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wadai ufirauni, watajirisha mapema
Hivyo mambo ya kigeni, yametunukiwa dhima
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Uwaonapo fuoni, nusu uchi wa mnyama
Watu hawana imani, umezidi uhasama
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama sodoma!
Na viongozi wa dini, kuabudu darahima
Wamekeuka yamini, kati yao na Rahima
Wamemuasi Manani, na kusahau kiyama
Yafanana na sodoma, miji yetu kwa yakini.

Miji yetu kwa yakini, kidogo kama Sodoma!
Wamemuasi manani, na kusahau kiyama
Ya Illahi tuauni, tuwe watu maamuma
Tukue katika dini, siku zetu za uzima
Yafanana na Sodoma, miji yetu kwa yakini.

## MASWALI

**(a)** Bainisha bahari ya shairi hili ukijikita katika ruwaza zifuatazo **(alama3)**

**i)** Mishororo
**ii)** Maneno
**iii)** Vina

**(b)** Eleza muundo wa shairi hili **(alama4)**

**(c)** Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili **(alama3)**

**i)** Tashbihi
**ii)** Taswira
**iii)** Tasfida

**(d)** Eleza toni ya shairi hili **(alama1)**
**(e)** Bainisha nafsi nenewa katika shairi hili **(alama1)**
**(f)** Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili **(alama2)**
**(g)** Andika ubeti watatu kwa lugha tutumbi **(alama4)**
**(h)** Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi **(alama2)**
i) Manani
**ii)** Marijali

## SEHEMU B: RIWAYA

**A.Matei:** *Chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au la 3*

**2.** "Nakumbuka asubuhi ya pili baada ya mtafaruku kuanza.Nilikuwa sebuleni na mwanangu tukitazama runinga".

**(a).** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
Eleza nafasi ya msemaji katika kuwakuza wahusika wengine riwayani **(alama 5)**
**(b).** Tambua mbinu kuu ya kimtindo uliotumika katika dondoo. **(alama 1)**
**(c).** Eleza jinsi mbinu uliyotaja hapo juu (iii) (a) ilivyotumika kukuza maudhui riwayani **(alama 10)**

**3.** Madhila anuwai yanayowazonga wahusika wengi katika riwaya ya Chozi La Heri yanafungamanishwa na hiari ya maamuzi yao. Jadili. **(alama 20)**

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**P.Keya***: Kigogo*

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "Ama kweli dunia gunia . Ilikumeza hindi bichi ikakuguguna, sasa inakutema guguta."
**(a).** Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama4)**
**(b).** Eleza mbinu mbili za kimtindo katika dondoo. **(alama2)**
**(c).** Masaibu yanayowakumba wahusika katika Kigogo ni zao la matendo yao ya awali. Fafanua kauli hii kwa kutolea mifano mwafaka tamthiliani**.** **(alama 14)**

5. Ubinafsi una athari kubwa katika jamii. Tetea kauli hii kwa kutolea hoja ishirini kamilifu katika tamthlia ya Kigogo. **(alama 20)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**A.Chokocho Na D.Kayanda:** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

*K. Wasike***: "**Mapenzi ya Kifaurongo"

6. Looh! Kwani swali langu liko vipi? Kwa nini wanafunzi wanacheka? Dkt. Mabonga hacheki safari hii kwa nguvu. Haikosi nimemuudhi.

"Hilo si swali," anasema. "Iwapo ulinuia kuchekesha ungenyamaza tu. Hatukuja hapa kuchekeshwa. Tena pale ulipo hujui kuchekesha."

**(a).** Bainisha mbinu za kimtindo zilizotumiwa kwenye dondo. **(alama6)**

**(b).** "Hadi sasa mimi ni kama rubani aliyeharibikiwa na ndege angani." Eleza maana ya kitamathali inayojitokeza kwenye kwenye dondoo hili. **(alama14)**

*S. A. Mohamed:* "Tumbo Lisiloshiba"

**7.** (a)"Fujo hazitatuhamisha hapa panapo ardhi yetu."

Kwa kurejelea kauli hii jadili namna ambavyo wanyonge katika hadithi ya Tumbo Lisiloshiba walivyojiopoa kutoka kwadhulma za uongozi mbaya. **(alama8)**

(b) Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili nafasi ya Elimu katika Jamii. **(alama12)**

**i)** Mapenzi Kifaurongo

**ii)** Shogake dada ana ndevu

**iii)** Mame Bakari

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**(a).** Eleza maana ya semi katika Fasihi Simulizi. **(alama2)**

**(b).** Fafanua sifa sita za semi. **(alama6)**

**(c).** Wewe ni mwigizaji wa michezo ya jukwaani. Eleza mambo sita ambayo utazingatia ili kufanikisha uigizaji wako. **(alama6)**

**(d).** Onyesha jinsi methali ni utanzu tegemezi kwa kueleza miktadha ambapo hutumiwa. **(alama 6)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 7 PAPER 1

**NAME…………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## MASWALI

**1. LAZIMA**

Mwandikie barua mhariri wa Gazeti la Baraka ukimweleza sababu za watoto wengi katika kaunti yako kuacha shule na kujiingiza katika ajira za mapema.

**2.** Vipakatalishi vimeleta manufaa mengi nchini .

Fafanua.

**3.** Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali:\

Mcheka kilema hafi bila kumpata.

**4.** Andika kisa kitakachoanzia kwa maneno yafuatayo:

Kushoto kulikuwa na jitu la miraba minne ambalo lilitema cheche za matusi ungedhania ni karakana …

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 7 PAPER 2

**NAME…………………………………………………. INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN………………………**

**DATE………………………………………**

**SEHEMU YA A: UFAHAMU** **(alama 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali***

"Swala la idadi kubwa ya watoto wadogo wanaoendelea kumiminika mijini na kuonekana wakiranaranda mijini ovyo,halijapewa umuhimu wowote wa haja na serikali za nchi nyingi,licha ya mijadala katika warsha anuwai,zilizofanyika kujadili swala hili nyeti.

Kwa kutokuwa na sheria ama sera iliyo wazi kuhusu haki na usalama wa watoto,sarikali zetu hazina budi kukubali kubeba uzito wote wa lawama. Hii ni kwa sababu, serikali zetu zimelipuuza na kuvalia miwani swala hili kwa kuchukulia kuwa litapotea lenyewe katika hewa yabisi. Yafaa ifahamike kuwa usalama wetu katika siku zijazo utategemea jinsi tutakavyolikabili ana kwa ana tatizo hili wakati huu. Wakati wa kutenda ni sasa. Aidha, watoto hawa wanaokulia mitaani bila malezi,maelekezo wala mwongozo mwafaka wa kimaisha, wanakua bila mapenzi hivyo hawajui maana ya kupenda. Wanachokijua ni chuki na haja ya kulipiza kisasi didhi ya jamii iliyowachonga jinsi walivyo. Hawajali lolote hata kifo. Wako tayari kujikabidhi kwa haini yeyote mwenye nia mbaya,bila kujali matokeo, muradi tu, wapate riziki.

Tunapendekeza kwa serikali, washika dau kama vile mashirika ya kujitolea, viongozi wa dini, shule, vyuo na wananchi kwa jumla wachange bia katika kutafuta mikakati ya kulitatua tatizo hili kabla halijageuka kuwa janga la kijamii ambalo tutashindwa kulimudu. Mpango wa vijana hawa kujiunga na huduma ya taifa ni jambo linalofaa kutiliwa maanani.

Tunapendekeza makao Zaidi ya watoto wanaozurura mijini yajengwe ambapo watapata mafunzo ya kiufundi yatakayowawezesha kujitegemea maishani. Badala ya kulitegea mgongo swala hili, serikali zinawajibika kuwasajili hawa watoto ili waweze kuunganishwa na familia na koo zao. Utafiti uliofanywa na wataalamu wa Elimu jamii umebainisha kuwa ni asilimia kumi tu ya watoto hawa wa mitaani wasiokuwa na mahali wawezapo kupaita

nyumbani. Asilimia tisini iliyobaki, angalau wana mahali wanapoweza kupaita nyumbani ilhali wanaendelea kuwa mitaani. Wazazi tumesahau wajibu wetu. Wengi wetu tumelikimbia jukumu la ulezi tulilopewa na muumba. Hawa waliojipaka masizi mwilin mzima, wanaozurura ovyo mitaani, si matokeo ya maumbile;hawakuja duniani kwa sadfa, hawakuulizwa wala kushauriwa. Makosa ni yetu wazazi. Tuliwaleta hapa duniani, kisha tukawakimbia.Hatutasamehewa duniani na akhera.

Mwenye njaa hana miiko. Ili kijiruzuku, hawa watoto daima wanachumia jaani.Kwa kudura ya jalia, huenda siku moja watalia kivulini. Asiyekuwa na wake ana mungu.Aghalabu, watoto wanaozurura mitaani hupewa pesa na wafadhili. Wakati mwingine wanaiba. Maisha haya ya kuomba au kuiba wanaona yanaridhisha Zaidi kuliko kumenyeka na kazi ya kibarua kutwa kucha. Kwa bahati mbaya, watoto hawa wamatumia pesa wanazopata kutoka kwa wafadhili kujichimbia kaburi. Aidha pesa wanazopatiwa watoto hawa wanazitumia kununulia gundi badala ya chakula.

Wafadhili wanashauriwa wawape chakula hawa watoto badala ya pesa taslimu. Kusema kweli, unapompa mtoto wa mitaani pesa,utakuwa unainua biashara ya mwenye kiwanda cha gundi,jambo ambalo litakuwa sawa na kuweka sahihi mkataba wa kifo cha mtoto mwenyewe.

Wataalamu wa afya wanaonya kuwa gundi ikivutwa kwa muda mrefu inaweza kusababisha upofu au kifo.Wataalamu hawa wanazidi kutuarifu kuwa matumizi ya muda mrefu ya gundi huathiri ubongo,figo na maini. Mtumiaji pia anaweza kupoteza uwezo wa kutembea na hata kupooza kabisa.

Sababu wanazotoa hawa watoto ni kwamba, uvutaji gundi,huwaondolea njaa,baridi ya usiku na kuwatuliza mawazo. Ni jambo la kusikitisha kwamba tunaendelea kushuhudia bila kujali hawa watoto ambao ni kiungo cha jamii yetu,wakijiangamiza. Wananchi kwa ujumla hawaha budi kuhamasishwa dhidhi ya athari ya matumizi ya gundi.Wafanya biashara wanaowauzia watoto hawa gundi yafaa wakome,la sivyo wachukuliwe hatua.Kutolitatua tatizo hili la watoto wa mitaani hivi sasa,kutapeleka kuwako kwa kizazi cha mitaani ambacho kitazaliwa mitaani,kulelewa mitaani,kuoa mitaani na kufia mitaani.Kadiri mataifa yanavyoendelea kujitia hamnazo kuhusiana na swala hili,ndivyo tunavyokubalia jinai itawale,sasa na wakati ujao.

Hawa watoto watakapokua,watageuka kuwa wapigaji watu kabari,majambazi,wezi wa kutumia nguvu ama watatumiwa na mahaini kutimiza uhaini wao.Hawa watoto wenye njaa,watalazimika hatimaye,kuwatoa wenywe shibe tonge mdomoni.Matokeo ya hali hii ni kwamba katika siku zijazo,hawa ndio watu watakaotunyima starehe ya kulala unono.Watatuchafya mitaani,majumbani,vijijini na kutuvizia mabarabarani.Tuna sababu nzuri ya kutiwa hofu na tatizo hili,kwani jinsi kizazi kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu.”

## MASWALI

**(a)** Taja jambo moja linalochangia kuweko kwa watoto wanaorandaranda mitaani. **(alama 1)**

**(b)** Maisha ya mitaani huathirije watoto? **( alama 3)**

**(c)** Tatizo la watoto wanaorandaranda mitaani laweza kutatuliwaje? **(alama 3)**

**(d)** Eleza maana ya: **(alama 2)**

i. Hawa watoto wanachumia jaani

ii. Jinsi kizazi cha mitaani kinavyozidi kupanuka,inaonekana tumelitega bomu ambalo litakuja kutulipukia usoni mwetu. **(alama 2)**

iii. Mwenye njaa hana miiko. **(alama 2)**

**(e)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye taaria: **(alama 2)**

i. Aidha:

ii. Gundi:

## 2.UFUPISHO:(ALAMA 15)

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo***

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri na kufahamu ugumu wa usemi. Twajifunza matumizi ya lugha katika kuzungumza na kuwasikiliza wengine wakizungumza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumza kama vila michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidia katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile ilivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka au amefiwa, haya yote ni ujuzi. Wakati juao mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambae amepatikana na mambo kama huyo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi. Fauka ya hayo , karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inambidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu ya taaluma fulani anayojifunza . Inafaa asome juu ya michezo, mambo ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

**a)** Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)
Matayarisho
Jibu

**b)** Kwa kuzingatia habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho(Maneno 30) (alama 5 utiririko)
Matayarisho
Jibu

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**(a)** Toa mifano miwili miwili ya **(al.2)**
i. Sauti ghuna ambazo ni vipasuo ………………………………………….………..
ii. Sauti sighuna ambazo ni vikwamizo ………………………

**(b)** Onyehsa mofimu katika neno Aliyemcha **(al.2)**

**(c)** Andika sentensi yenye muundo ufuatao **(al.2)**
KN(W+V) + KT (t +RH)

**(d)** Tumia neno shirika kama nomino na kama kielezi katika kutunga sentensi moja **(al.2)**

**(e)** Kwa kutunga sentensi vumisha nomino nguruwe kuwa kivumishi cha idadi bainifu. **(al.1)**

**(f)** Andika sentensi ifuatayo katika hali ya kutendewa **(al.1)**
Mtoto wa waziri amekufa

**(g)** Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu wingi **(al.2)**
Msomi hakutuzwa siku hiyo

**(h)** Tunga sentensi moja inayobainisha maana mbili tofauti za neno chuma **(al.2)**

**(i)** Tambua kiima na aina za yambwa katika sentensi ifuatayo**.** **(al.4)**
Mwalimu mkuu hupigiwa nguo pasi na Maria

**(j)** Kwa kutumia mifano mwafaka fafanua miundo yoyote miwili ya kirai nomino **(al.2)**

**(k)** Andika sentensi ifuatayo kwa wingi **(al.2)**
Mgeni huyo na mwingine walikula wali kwa uma

**(l)** Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja **(al.1)**

**(m)** Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika udogo wingi **(al.2)**
Ng'ombe wangu ana ndama mdogo

**(n)** Tunga sentensi zenye mipangilio ifuatayo; **(al.4)**
i. Kishazi tegemezi na kishazi huru
ii. Kishazi tegemezi na kishazi tegemezi

**(o)** Eleza matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo: **(al.3)**
Nyamunga na kitoto wamekuwa wakila, wakiimba kikasuku

**(p)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. **(al.4)**
Mtoto wa mjomba alikuja kwetu nyumbani jana

**(q)** Andika kwa msemo wa taarifa. **(al.2)**
'Yafaa tumwendee mama mkubwa ili atushauri juu ya jambo hili,' Amina alipendekeza.

**(r)** Andika kinyume cha: **(al.1)**
Chakula hiki kitamu nitakimeza

**(s)** Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo. **(al.2)**
(i) Kiwakilishi nafsi huru
(ii) Kiwakilishi nafsi kiambata

## ISIMUJAMII (alama10)

**(a)**Tofautisha kati ya kuhamisha msimbo na kuchanganya msimbo. **(alama 2)**

**(b)**Taja mambo mawili yanayochangia katika uhamishaji msimbo. **(alama 2)**

**(c )**Taja kaida mbili zinazotawala maamkizi katika jamii huku ukitoa mifano mwafaka. **(alama2)**

**(d)** Fananisha sifa zozote nne za sajili ya maabadini na mahakamani. **(alama 4)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 7 PAPER 3

**NAME…………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## SEHEMU YA A: TAMTHILIA

**P.Kea:Kigogo**

1. ***Lazima***

(a)Jadili jinsi kumi ambazo maudhui ya ukatili yanajitokeza katika Tamthilia ya Kigogo **(alama 10)**

(b)Eleza mifano kumi ya matumizi ya kinaya katika Tamthilia ya Kigogo. **(alama 10)**

## SEHEMU YA B

**RIWAYA: CHOZI LA HERI**

*(Assumpta K. Matei)*

Jibu swali la Pili au la Tatu

2. “Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni…”

a) Eleza muktadha wa maneno haya. **(alalama 4)**

b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. **(alama 2)**

c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. **(alama 6)**

d) Thibitisha kuwa hakuna usawa baina ya wanadamu. **(alama 8)**

**Au**

3. Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Hari:

(a) Hotuba **(alama 10)**

(b) Uozo katika jamii **(alama 10)**

## SEHEMU C

**HADITHI FUPI**

(Mtihani wa maisha)

'Leo mwalimu mkuu atajua kwamba mdharao biu hubiuka'

(a)Eleza muktadha wa maneno haya. **(Alama 4)**

(b)Taja mbinu ya lugha iliyotumika katika mktadha huu. **(Alama 6)**

(c)Eleza wasifu wa mzungumzaji wa maneno haya. **(Alama 2)**

(d)Jadili maudhui ya elimu kama yanavyojitokeza katika hadithi hii. **(Alama 8)**

(Ndoto ya mashaka (Ali Abdulla)

**(5)** 'Kusema kweli lakini hata mimi sikuwa na nadhari katika kumpenda msichana huyu … Nilimpenda kufa! Lakini! Kwao bure tu!'

(a) Eleza mkutadha huu. **(Alama 4)**

(b)Taja mtindo wa lugha uliotumika katika mkutadha huu. **Alama 4**

(c) Taja sifa mbili za mzungumzaji. **(Alama 2)**

(d) Onyesha maudhui ya umaskini katika hadithi fupi ya Ndoto ya mashaka.

## SEHEMU YA D

***USHAIRI***

*Jibu swali 6 au 7*

(6) **USHAIRI**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.
Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu;
Ni miti yote hujipinda migongo

Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha ha …
Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho;
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutokujua
Laiti angalijua, laiti angalijua!

## MASWALI

(a)Eleza matatizo manne yanayompata mzungumziwa. **(Alama 4)**
(b)Eleza mtindo wa lugha uliotumiwa na mshairi na utoe mifano. **(Alama 8)**
(c)Taja nafsineni katika shairi hili. **(Alama 1)**
(d)Eleza toni ya shairi hili. **(Alama 1 )**
(e)Taja mbinu mbili za uhuru wa kishairi uliotumika na utoe mifano. **( Alama 2)**
(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. **(Alama 4)**

**(7)*Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Leo kitaka nifike, natamani, ila wauma mwili
Kwa kazi nihusike, samahani, unahiliki mwili
Napenda nihesabike, makundini, ila huwezi mwili
Vitisho pamwe kelele, ninavicha, kwa nafsi na mwili
Ila ugonjwa utimile, umechacha, na kuudhili mwili
Msikose simile, magalacha, si gurudumu mwili.
Vingekuwepop viraka, kuutia, ngeushuruti mwili
Kifundi kivipachika, kuingia, hata kuridhi mwili
Upya ukaungilika, kuvutia, roho na wake mwili.
Lakini kamwe haiwi, kuvipata, vipande vyake mwili
Sihofu kupata mawi, sitajua, kupigania mwili
Hata kufutwa sikawi, nitakita, kidete nao mwili.

Kazi ninaithamini, ni hakika, akilini na mwili
Ila kamwe siamini, kusagika, damu, jasho na mwili
Uwele hususani, kioneka, nguvu hitishi mwili.

## MASWALI

(a)Liweke shairi hili katika bahari tatu. **(Alama 3)**

(b)Eleza dhamira ya mshairi. **(Alama 2)**

(c) Eleza muundo wa shairi hili. **(Alama 4)**

(d) Toa mifano ya uhuru wa kishairi uliotumika. **( Alama 4)**

(e)Eleza kwa kifupi maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. **(Alama 3)**

(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari. **(Alama 4)**

## SEHEMU D

### FASIHI SIMULIZI

A(i) Miviga ni nini? **(Alama 2)**

(ii) Eleza sifa nane za miviga. **(Alama 8)**

B (i) Ulumbi ni nini? **(Alama 2)**

(ii)Eleza sifa nane za ulumbi **(Alama 8)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 8 PAPER 1

**NAME…………………………………………………. INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

## MASWALI

1. **LAZIMA**
   Wewe ni katibu wa chama cha waandishi habari chipukizi shuleni kwako. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika mnamo Oktoba 27, 2022

2. Fahali wawili wapiganapo ziumiazo ni nyasi.

3. "Sayansi na ufundi zina nafasi muhimu katika kuafikia ruwaza ya mwaka 2030 ya maendeleo ya taifa. Jadili

4. Andika insha itakayomalizika kwa: …

Nilishangaa kugundua kuwa nilikuwa nimeokotwa msituni siku kumi baada ya mkasa huo.

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 8 PAPER 2

NAME………………………………………………… INDEX NO…………………

SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………

DATE………………………………………

1. **UFAHAMU** (*alama 15*)

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswahi yanayofuatia.***

Mengi yamsesemwa kuhusiana na nchi kuwa na katiba mpya. Kile ambacho hakibainiki hasa, ni jinsi ambavyo wanasiasa wetu, wamejitwalia nafasi ya ukunga na tena ya uzazi na mama mwenye mtoto kutupwa pembeni. Je, huyu si mtoto wa wanjiku tena? Huenda visa vya hivi karibuni vinavyohusu familia mbalimbali vikawa na mzizi katika huy mwan wa wanjiku. Si haba unasikia kisa cha baba ambaye amemwua mwanawe na kumkatakata vipande vipande na kuyaacha yaoze yakiozeana kwa sababu ya msinyo au msakamo. Akili za binadamu zinapolazimishwa kwenda zaidi ya uwezo wa kawaida, matokeo aidha huwa ni kuingiwa nao wazimu, yaani kupagawa au kuua bila kukusudia.

Aidha kuna wengi ambao huyachukua maisha yao wenyewe kwa kutaka kuondokewa na shida. Hawa husahau kuwa mbio za sakafuni huishia ukingoni. Si nadra kwa hivyo kuwa na viumbe wanaojitia kitanzi mara kwa mara ili kuepuka mng'ang'ano wa maisha yasiyo na tumaini katu. Je, hali hii itandelea hadi lini?

Muujiza mwingine ni ule wa ubakaji wa watoto na maajuza. Nyanya tena si mpenzi aliyekusanyiwa watoto wa vijana wa kata nzima jioni na wakauzunguka moto wake, na kushiba ngano zake ambazo zilikuwa hazina mwisho. Si nyanya ambaye zao lake kuu likikua viazi vitamu na njugu karanga kwa minajili ya kuwalisha wajukuu wake jioni, na asubuhi kama ndege kuonja umande wa asubuhi? Leo nyanya anaishi kwa woga, hawaamini tena wajukuu. Ni wababakaji. Sasa vipi chemichemi ya furaha kugeuzwa simanzi ya huzuni? Wasemao husema dunia uwanja wa fujo.

Ukizuru magereza yetu ndipo utajua tuna shida katika nchi yetu. Watu wamefungiwa tumbitumbi. Hadithi zao nazo ni nyingi: Uvutaji bangi, wizi wa kimabavu, kuua jamaa, uchopozi na zaidi. Hakuna mwisho

Ashakum si matusi, ugonjwa wa "Kidon" umeanza kuwashika ndugu zetu vilivyo. Asilimia ya watu wanashikwa wakilangua dawa za kulevya haisemeki. Wote huwa na jibu lile lile. Maisha yamekuwa ghali na hapana ila kutumia kila mbinu. Je, hatujaambiwa uhalifu haulipi chochote?

Kukariri usemi huo wa Leoruad mambo mbotela na wengine wengi wenye semi kama hizo wakiwepo wahubiri mbalimbali ni baraka maana hupunguza makali ya maisha na kutoa nafasi ya kutabasamu kidogo, ijapo siku moja.

## MASWALI

**(a)** Dokeza visa vyovyote vinavyoonyesha msinyo kulingana na makala **(Alama 3)**

**(b)** Mwandishi wa makala anawalaumu wanasiasia kwa nini? **(Alama 2)**

**(c )** Nyanya alikuwa na wajibu upi kulingana na kifungu hiki? **(Alama 2)**

**(d)** Fafanua "Ugonjwa wa Kidon" **(Alama 2)**

**(e)** Eleza ni kwa jinsi gani wajibu wa nyanya umegeuzwa na vijana wenyewe. **(Alama 2)**

**(f)** Fafanua msamiati huu kama ulivyotumiwa kwenye makala. **(Alama 4)**

**(i)** Tumbitumbi

**(ii)** Chemichemi

**(iii)** Ashakum si matusi

**(iv)** Wanjiku

## 2. MUHTASARI. (ALAMA 15)

***Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali yanayofuata.***

Nchi nyingi duniani zimetia saini mkataba wa umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Haki ni mambo mema ambayo watoto wanastahili kutendewa. Kwa kutia saini nchi hizi zimetangaza kujitolea kwao kuzilinda na kuhakikisha kuwa hakuna ukiukaji wake na kuwa watoto wote katika hilaya zao wananufaika kutokana na haki zao.

Miongoni mwa haki hizi ni kuwa kila mtoto ana haki ya kuishi na kupata chakula cha kutosha na chenye viinilishe bora. Pili, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu hii inafaa kutolewa bila ada na iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi; kisha kila mtoto ana haki ya kutopigwa na kutodunishwa kwa namna yoyote, iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vinginevyo. Mtoto ana haki pia kutolazimishwa kufanya kazi za kiutumwa, nzito na za kushurutishwa. Halikadhalika, ana haki ya kuishi katika nyumba au makazi bora na salama, kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Anatakiwa ashirikishwe katika kufanya maamuzi. Fauka ya haya, ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum, michezo, upendo na habari. Isitoshe, anastahili kuheshimiwa kimawazo

na kihisia. Haki hizi zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, hivyo serikali za mataifa zimeshirikisha haki hizi katika katiba za nchi zao na sheria zao.

Walakini, haki hizi, bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. La kusikitisha na kukera ni kuwa wanaotarajiwa kuwa vigogo wa kuzilinda haki hizi ndio wanaongoza kuzikiuka. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi kipunda, kuteswa, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Kuna watoto wengi wanaolala nje. Wengi hawapati chakula; licha ya kuwa wanatakiwa kupata chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi kwani hata awamu moja moja ni adimu kupata.

Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Viongozi katika mataifa haya hawafanyi kitu ila kutazama tu wakati watoto wanaotakiwa kuwalinda, wanageuzwa kuwa mibaba ya kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia huvalishwa mabuti ya kijeshi ambayo ni mizigo mizito ya kubeba. Mbali na bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani wakati wanatakiwa kuwa wamelindwa majumbani na shuleni na wazazi wao na serikali.

Jukwaa la vijiji vya mataifa ya ulimwengu wa tatu limesheheni watoto wasioenda shule kwa sababu ya lindi la ufukara uliokithir. Elimu ya bure inayogusiwa katika haki za watoto haipo. Wanaong'ang'ana iwepo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana. Jiulize, watoto wangapi sasa hivi wamo majumbani bila kwenda shuleni kutokana na ukosefu wa karo? Wangapi wamo mitaani wakivuta na kunusa gundi huku wakiombaomba vishilingi?

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima na kuungana mikono kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu haki za watoto. Twapasa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati bali si kwa chati.

## MASWALI

(a) Fupisha aya mbili za kwanza **maneno (65-70**)

(Alama 8,Utiririko 2)

**Matayarisho**

**Jibu**

(b) Eleza ni vipi ukiukaji wa haki za watoto unaweza kuepukwa. (Maneno 30-35) (Alama 1,Utiririko 1)

**Matayarisho**

**Jibu**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (*alama* 40)

***(a) Taja mojawapo ya sauti zifuatazo*** **(Alama2)**

i) Nazali……………………………………………………………………….

(ii) Kipasuo cha kaa kaa laini……………………………………………………

***(b) Andika kwa usemi wa taarifa.***

"Hivi vibanda vilivyo kando ya shule yetu vinatumiwa kulanguzia dawa za kulevya" Mwalimu mkuu alilalamika. **(Alama 3)**

***(c ) Akifisha.***

Ah mbona hutaki kuandamana naye. **(Alama 2)**

***(d) Andika kwa kuzingatia maagizo*** **(Alama 2)**

Polisi mwoga akishindwa kumshambulia mwizi kwa kuhofia kutupiwa risasi.

Anza: Woga……………………………………………***Bainisha aina za yambwa*** **(Alama 1)**

Amina alimtungia mashairi mchumba wake.

***(e) Bainisha aina za virai kwenye sentensi ifuatayo***

(Alama 1) Leo asubuhi nilichelewa kuja kazini

***(f) Tumia mishale kuchanganua sentensi ifuatayo:***

(Alama 4) Mtoto aliutupa mpira uliokuwa mbaya.

***(g) Andika kwa udogo – wingi***.

**(Alama 2)** Nyoka aliyekuwa na mkia mrefu aliingia nyumbani

***(h) Tunga sentensi ukitumia; nomino ya wingi*** **(Alama 1)**

**(iii)** ***Onyesha matumizi ya kivumishi cha pekee katika sentensi ifuatayo:*** **(Alama 1)**

Wanafunzi wengine walipelekwa hospitalini

***(j) Kwa kurejelea ngeli za mahali, andika sentensi tatu ukionyesha matumizi ya kila moja*** (Alama 3)

***(k) Andika katika kauli ya kutendama.***

**(Alama 2)** Serikali ina mambo mengi ambayo yamefichwa.

***(l) Yakinisha sentensi ifuatayo.*** **(Alama 2)**

Wahudumu wasipopokea mishahara yao kesho hawatasherekea Krismasi kwa furaha.

***(m) Unda nomino dhahania kutokana na maneno haya.*** **(Alama 2)**

(i) Dhulumu……………………………………………

(ii) Kanusha…………………………………………………

***(n) Bainisha matumizi ya viambishi 'ndi' na 'ji' katika sentensi zifuatazo.***

(Alama 2) (i) Sisi ndisi wenye shamba hili

(ii)Mtoto amejikata kidole.

***(o)*** ***Tunga sentensi itakayodhihirisha "Ka" ya amri na ya ukariri wa vitendo.*** (Alama 4)

***(p)*** ***Ainisha mofimu katika neno lifuatalo*** **(Alama 3)**

Aliyefiwa

***(g)*** ***Andika kwa kinyume*** **(Alama 1)**

Hii ni njia nyembamba

***(v)*** ***Tumia 'o'- rejeshi badala ya 'amba'*** **(Alama 2)**

Mtu ambaye hufungwa ni yule ambaye huhalifu sheria.

## 4. <u>ISIMU JAMII *(alama10)*</u>

1. "Mheshimiwa spika naomba nipewe fursa kutoa maoni yangu kuhusu hoja iliyowasilishwa…"

**(a)** Weka makala haya katika muktadha wake. **(Alama 2)**

**(b)** Eleza sifa za mazungumzo yanayofanywa katika muktadha huo uliotajwa. **(Alama 8)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 8 PAPER 3

NAME………………………………………………… INDEX NO…………………

SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………

DATE………………………………………

**SWALI LA KWANZA, SWALI LA LAZIMA**

**SEHEMU YA A: USHAIRI- (Alama 20)**

Niokoa muokozi, uniondolee mashaka
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekitiri simanzi,ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka,nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka,nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka,nami nipate pumua
Naomba hisikitika,na mikono hiinua
Mtenda ndiwe moliwa,nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe moliwa,we ndiwe mola wa anga
Mazito kuyaondoa,pamoja na kuyatenga
Ukauepusha ukiwa,ya pingu zilonifunya
Nikundulia muwanga,nipate niyatakayo

Nikundulia muwanga,nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea,itoke kwangu moyoni
Mambo mema niegheshea,maovu nisitamani
Nitendea wa manani,nipate niyatakayo

Igeuze yangunia,dhaifu unipe mema
Nili katika dunia,kwa afia na uzima

Moliwa nitimizia,yatimize yawe mema
Nifurahike mtima,nipate niyatakayo.

## MASWALI

**(a).** Eleza bahari zozote mbili za shairi hili **(alama 4)**
**(b).** Eleza muundo wa shairi hili **(Alama 4)**
**(c).** Mshairi ametumia uhuru wake wa utunzi. Eleza mifano minne huku ukitoa mifano **(alama 4)**
**(d).** Andika ubeti wa pili katika lugha tutumbi **(alama 4)**
**(e).** Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili **(alama.2)**
**(f).** Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi **(alama 2)**
(i). Nimedhihika
(ii). Nifurahike mtima

## SEHEMU B: RIWAYA – ASSUMPTAMATEI - CHOZI LA HERI

**2.** Haki za watoto hazitiliwi maanane katika jamii nyingi za kiafrika. Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya chozi la heri **(Alama 20)**

**au**

**3.** "Kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika" **(Alama 20)**
a. Eleza muktadha wa dondoo hili **(Alama 4)**
b. Eleza namna msemaji alivyoukata mkono aliostahili kuuibusu. **(alama 6)**
c. Eleza tamathali ya usemi unaojitokeza katika dondoo hili. **(alama.2)**
d. Fafanua sifa nne za msemaji wa kauli hii **(alama 8)**

## SEHEMU C: TATHILIA KIGOGO NA PAULINE KEA

4. ''Na hawa wafadhili wao nao lazima wavunje kambi zao. Sagamoyo twajiweza''
a. Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**
b. Kwa kutolea mifano saba kwenye tamthilia eleza jinsi kauli hii ''Sagamoyo twajiweza'' ni kinaya ? **(alama 14)**
c. Mbali na kinaya tambua mbinu nyingine ya kisanaa katika dondoo hili **(alama 2)**

**AU**

5. Jadili mbinu wanazotumia wanasagamoyo kujikomboa kutoka utawala dhalimu wa Majoka **(Alama 20)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI - TUMBO LISILOSHIBA

6. "… Ningeondoka…..mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana"

**a)** Eleza muktadha wa maneno haya **(Alama 4)**

**b)** Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili **(Alama 2)**

**c)** ''Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa **(Alama 9)**

d). Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii **(alama.5)**

**AU**

**7. (a).** Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa **(alama 13)**

(b). Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza,eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza **(alama 7)**

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8 (a)** Miviga ni nini? **(Alama 2)**

(b) Fafanua sifa sita za miviga **(Alama 6)**

(c) Kwa nini jamii huthamini miviga **(Alama 8)**

(d). Onyesha udhaifu unaohusishwa na miviga **(Alama 4)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 9 PAPER 1

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL…………………………………………  SIGN………………………**

**DATE……………………………………**

## MASWALI

1. **LAZIMA**

Andika wasifu wa ndugu yako ambaye anakaribia kuustaafu hivi karibuni.

2. Andika insha kuhusu umuhimu wa vijana katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa.

3. Tunga kisa kinachodhihirisha maana ya methali ifuatayo.

   Chombo cha kuzama hakina usukani.

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno yafuatayo:

   Tulijifunga kibwebwe kuwaopoa wahasiriwa waliokuwa wamefunikiwa na vifusi vya maporomoko ya jengo hilo lakini juhudi zetu ziliambulia patupu.

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 9 PAPER 2

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………**

**DATE………………………………………**

**1. UFAHAMU (Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Vijana waliombeba Naeku juu juu walipoingia uani mwa Mzee Laboyo walilakiwa kwa shangwe na vigelegele vilivyotoka vinywani mwa wanawake wachache waliokuwa pale. Bila shaka walialikwa makusudi ili kumlaki Naeku. Vijana hao walimteremsha Naeku ambaye alisesereka kutokana na uchovu mwingi. Ufyefye ulimvaa akajihisi kuwa mfungwa asiye na hatia. Huku michirizi ya machozi ikiwa ingali inabubujika toka machoni, wanawake hao walimwinua juu juu. Vicheko vya kusudi vilivyoandamana na riboribo za arusi vilipamba maskani ya Mzee Laboyo. Walimwingiza katika kijumba kilichokuwa mkabala na kasri la shaibu huyo na kushindika mlango.

Kijumba kile hakikuwa na vitu vya haja. Mlikuwa na viti viwili vidogo, kitanda kimoja cha msonobari kilichotandikwa maridadi kabisa. Mito minne ya rangi ya hudhurungi ilitulia juu ya kitanda hicho kilichofarishiwa matandiko ya mahameli. Katikati ya chumba hicho, kulikuwa na kijimeza cha mviringo kilichotandikwa kitambaa cheupe. Juu yake kulikuwa na bilauri pamoja na chupa iliyojaa maji.

Naeku aliketishwa kitandani baada ya kupakwa mafuta, huku akiwa bado anapigana nao ili kujiopoa. Kisha wanawake hao walitoka wakaukomelea mlango kwa nje, na kumwacha Naeku peke yake mle ndani.

Naeku aliacha kulia na kuvuta fikra ili ajue namna ya kupatoroka mahali pale. Hapa ndipo picha za matukio yaliyoandama kutoroshwa kwake zilipomjia akilini. Naam, sasa alielewa fika kwa nini wazee fulani walikuwa wakija nyumbani kwao mara kwa mara, kuongea na wazazi wake. Alielewa kwa nini ng'ombe na mbuzi walikuwa wakiletwa kwao jioni jioni na watu asiowafahamu.

Kila alipomuuliza mamake kuhusu mifugo hao, mama mtu alimjulisha kuwa walileltwa hapo kwa muda tu ili mwenyewe apate nafasi ya kujenga zizi kubwa zaidi la kuwasitiri. Naeku alipovuta fikra zaidi, lilimjia wazo jingine lililomshtua zaidi. Awali alimsikia mmoja wa wale vijana akitaja jina "shaibu". Mamangu eee! Alikuwa ameletwa kuwa mke wa Mzee Laboyo mwenyewe!

"Mimi niolewe na kikaramba yule! Labda niwe maiti," Naeku alijisemea moyoni, " Lazima nijinusuru kabla Mzee yule kuniharibia maisha," aliwaza.

Aliangaza angaza macho mle ndani na kuliona dirisha dogo lililofungwa kwa ndani. Hata hivyo, dirisha hili lilijengwa juu sana kiasi cha kwamba hata kama angekanyaga kiti ili kulifikia, ingekuwa kazi ya bure.

Huko nje, aliwasikia watu wakijishughulisha na kadhia za jioni. Giza lilikuwa linanyemelea taratibu, na hivi punde kijiji chote kingezama gizani. Alimsikia mkewe Laboyo**,** Bi Mariamu**,** akiwabembeleza ng'ombe wake kuingia zizini, huku Hamadi akipiga miluzi ili kuwahimiza zaidi, Hadi kufikia wakati huu, hajamsikia wala kumwona Mzee Laboyo mwenyewe.Alipokuwa akiwazia la kufanya, mlango ulifunguliwa taratibu, akaingia mzee mfupi, mnene, menye ndevu nyeupe mithili ya theluji. Mara moja, Naeku alimtambua kuwa ndiye Mzee Laboyo mwenyewe, kwani alishapata kumwona mahali mara kadha. Shaibu huyu alimtupia Naeku macho huku tabasamu limepamba usoni."Hujambo mpenzi?" Mzee Laboyo alimsalimu huku akimsogelea.Naeku alisimama ghafla na kumkabili, macho yakiwa yameiva kwa hasira."Sina jambo nikiwa nalo n'takwambia," alipasuka.

"Aaah, wacha hasira kinda wangu, karibu nyu…" Lakini kabla Mzee huyo hajamaliza alilotaka kusema, Naeku alidakia, "Niondokee mie! Tangu lini jizee kama wewe umri wa babu yangu ukawa mpenzi wangu? Ulidhani ulipopeleka zizi zima la mifugo kwetu na kuwamwagia wazazi wangu mapesa chekwachekwa, ungenifanya nikupende? Nakwambia umekula huu babu, hunipati leo wala kesho!"

Maneno ya Naeku yalimchoma Mzee Laboyo ambaye hakuzoea kujibiwa vile na mwanamke. Hasira zilianza kumnyemelea, zikapanda na kumsakama koo. Alifunua kinywa ili kutamka, lakini katu maneno hayakumtoka. Baada ya kupumua kwa nguvu aligugumia, "Ni…………nisubiri kidogo mpenzi………..naja hivi punde,,,,,,,tuyamalize usemayo." Kisha alichomoka mbio na kuufunga mlango kwa nje."Mawe! Labda tuyamalize nikiwa maiti! Katili mkubwa we!"Aliinuka pale alipoka na kuliendea lile dirisha. Aliliangalia kwa muda kisha akapanda juu ya kiti ili ajaribu kulifungua. Hakuweza kulifikia komeo ili afungue dirisha hilo."Lazima nitoke humu kabla jizee lile kuingia humu tena," alijipa moyo.

**MASWALI**

**(a)** Eleza namna mwanamke amenyanyaswa kwa mujibu wa kifungu hiki . **(ala 4)**

**(b)** Naeku alipinga mila dhalimu katika jamii yake. Thibitisha kwa kurejelea kifungu hiki. **(ala 3)**

**(c)** "Hujambo mpenzi?" Eleza kinaya katika maneno haya kulingana na kifungu hiki. **(ala 2)**

**(d)** Eleza taasubi ya kiume inayojitokeza katika aya ya kumi. **(ala 2)**

**(e)** Vijana wanachangia kuendeleza desturi zilizopitwa na wakati. Eleza kwa kurejelea kifungu. **(ala 1)**

**(f)** Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. **(ala 3)**

(i) alisesereka - ____________________________________________

(ii) kuvuta fikra ____________________________________________

(iii) nijinusuru ____________________________________________

## 2. UFUPISHO (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Miswada kadhaa imepitishwa ili kufanyia mageuzi sekta ya kilimo na kuboresha maslahi ya wakulima ambao wamehangaika kwa miaka mingi Waunda sheria wamejitokeza kuwatetea wakulima dhidi ya ushindani usio wa haki kutokana na wingi wa bidhaa zinazoagizwa kutoka mataifa ya kigeni ambazo huuzwa kwa bei duni. Mabadiliko hayo yatafaidi maelfu ya wakulima ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakilia kuhusu hasara wanayopata kutokana na kufurika kwa bidhaa kutoka nchi za kigeni, zinazouzwa kwa bei ya chini.

Kuanzia samaki, mayai, sukari, vitunguu na kadhalika, masoko na maduka ya jumla nchini yamekuwa yakijazwa bidhaa zinazoagiziwa kutoka mataifa jirani na kuwaacha wakulima nchini wakiwa hoi. Uimarishaji wa kilimo utachangia kuunda nafasi za ajira na kuimarisha viwanda jambo litakalowafaa maelfu ya vijana ambao wamekuwa wakilalamikia ukosefu wa ajira.

Hii ni hatua muhimu ikizingatiwa ni mojawapo wa Ajenda Nne Kuu za Rais Uhuru Kenyatta, kuhusu uongezaji thamani kwa bidhaa za kilimo. Japo juhudi hizo zinapaswa kupongezwa kwa kupatia kipaumbele maslahi ya raia, si jambo la kushangaza kwamba wabunge na wanasiasa wanaonekana ghafla kuanza kupatia kipaumbele maslahi ya raia.

Hii ni kwa kuzingatia kuwa msimu wa kampeni unakaribia kuhusiana na Uchaguzi Mkuu wa 2022. Katika juhudi za kutaka kuvutia wapiga kura ili wapate kuchaguliwa tena, wanasiasa hujitahidi kwa kila hali ikiwemo kuungana na kupitisha sheria ambazo huwafaidi wananchi na wakati mwingine kuwaathiri.

Hata hivyo, maamuzi hayo yanapofanywa kiholela kwa minajili tu ya kuvutia wapiga kura, baadhi ya sheria hizo huishia kuwaumiza wateja na uchumi na wananchi kwa jumla. Mfano mzuri ni kuhusu mswada wa Fedha 2021 ambao unahusu masuala mengi ya mwananchi wa kawaida kuanzia bidhaa kama vile pikipiki na shughuli za kilimo.

Kwa kuidhinisha sheria kuhusu kutozwa ushuru wa asilimia 16 wa VAT ikiwemo ada nyinginezo dhidi ya bidhaa za kigeni zinazoagizwa nchini, ni wazi kwamba bei ya bidhaa hizo itapanda na raia wengi hawataweza kumudu.

Isitoshe, hatua ya kuzuia ushindani kwa kufungia nje bidhaa za kigeni, pana tishio la wakulima na wenye viwanda nchini kulegeza kamba kuhusu viwango vya ubora na kuzalisha bidhaa duni. Hii ni kwa sababu wana hakika ya kupata soko bidhaa zao ziwe bora au vinginevyo hivyo, baadhi hawatajishughulisha mno na mwishowe, ni wateja tu watakaoumia kwa kukosa bidhaa bora. Ingawa juhudi za kuimarisha sekta ya kilimo zinafanywa kwa nia njema, ni sharti kuwe na tahadhari zisije zikaleta madhara zaidi kuliko manufaa.

## MASWALI

**(a)** Kwa maneno 85-90 fupisha aya ya kwanza tatu. (alama 7, 1, ya mtiririko).

Nakala ghafi

Nakala safi

**(b)** Eleza mambo muhimu yanayoibuka katika aya nne za mwisho. (maneno 90-95)
(ala 6, 1 ya mtiririko)

Nakala ghafi

Nakala safi

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

**(a)** (i) Eleza maana ya sauti mwambatano. **(ala 1)**

(ii) Toa mfano wa sauti mwambatano inayotamkiwa midomoni. **(ala 1)**

**(b)** (i) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi. **(ala 1)**

I + KKI + I

(ii) Andika neno lenye sauti zifuatazo:

Voweli ya nyuma wastani, kikwamizo ghuna cha ufizi na voweli ya chini wastani. **(ala 1)**

(iii) Eleza tofauti kati ya sauti /t/ na /d/. **(ala 1)**

**(c)** Andika upya kwa kufuata maagizo.

(i) Nyanya alijengewa nyumba maridadi na mjukuu wake. (Anza kwa kiima) **(ala 2)**

(ii) Tutamlipia mtoto ada kwa hundi. (Ainisha shamirisho) **(ala 3)**

(iii) Maji hayo yalinywewa na ngo'mbe wake. Andika katika hali ya kutenda) **(ala 2)**

**(d)** Eleza matumizi mawili ya kila kiakifishi . **(ala 4)**

(i) kibainishi

(ii) mkwaju

**(e)** Ainisha viambishi katika neno hili. **(ala 2)**

(i) mkobani

**(f)** Andika katika ukubwa wingi. **(ala 2)**

Kitanda hicho kilitumiwa na mtoto wake.

**(g)** Eleza matumizi ya ji katika sentensi hii. **(ala 2)**

Kijitoto hicho kilijing'oa mwiba chenyewe.

**(h)** Bainisha vivumishi. **(ala 2)**

Mwalimu mkulima alivuna maembe mengi.

**(i)** Tunga sentensi kudhihirisha upatanisho wa ngeli wa nomino kukimbia. **(ala 1)**

**(j)** Changanua sentensi kwa mtindo wa mchoro matawi. **(ala 3)**

Walishangiliwa walipowasili.

**(k)** Eleza matumizi ya na. **(ala 2)**

Mama na mtoto wake walilakiwa na naibu wa rais.

**(l)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao wa KN na KT. **(ala 2)**

KN(W) + KT(t + N)

**(m)** Unda nomino mbili kutokana na kitenzi nena. **(ala 1)**

**(n)** Jifya ni kwa figa, injika ni kwa ________________________________ na manati ni kwa ________________________________ **(ala 2)**

**(o)** Eleza maana ya msemo mkono wa birika. **(ala 1)**

**(p)** Ainisha vishazi katika sentensi hii. **(ala 2)**

Meza aliyonunua ni maridadi sana.

**(q)** Andika katika usemi wa taarifa. **(ala 2)**

"Kula tunda hili ulimalize," Amina alimwambia nyanya.

**4. ISIMU JAMII (ala 10)**

"Chenga chenga, chenga tena, aaaa baas! Goal! Habari ndio hiyo ndugu yangu!

(a) Tambua sajili hii. **(ala 2)**

(b) Huku ukitoa mifano, eleza sifa bainifu za sajili uliyotaja hapo juu. **(ala 8)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 9 PAPER 3

**NAME……………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL……………………………………… SIGN…………………………**

**DATE……………………………………**

## USHAIRI

**1.** ***Soma shairi kisha ujibu maswali***

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki.
Ukweli haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, akiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupumiwa zikatesa, wakizifuata nyago,
Hadi kwenye kwako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Pindi kinuna kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo
Tamko lake 'subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazi,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Aliye faraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kudai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchumbiye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo,

Bahati ni hadaa, kukupa alo sodawi, alibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi,kuvunja kaniyo,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa mazito kuambiwa,
Ama nitumie mbio, faudini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tama, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

## MASWALI

**(a)** Lipe shairi hili kichwa mwafaka. **(ala 1)**

**(b)** Eleza sababu ya mtungaji kulalamika katika shairi. **(ala 3)**

**(c)** Fafanua umbo la shairi hili. **(ala 3)**

**(d)** Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. **(ala 4)**

**(e)** Taja mifano miwili ya tamathali za usemi. **(ala 2)**

**(f)** Eleza maana ya. **(ala 2)**

(i) zani

(ii) faraghani

**(g)** Eleza kwa mifano mwafaka jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa katika shairi hili. **(ala 4)**

**(h)** Eleza bahari ya ushairi katika shairi hili. **(ala 2)**

**(i)** Taja nafsi neni katika shairi hili. **(ala 1)**

## RIWAYA YA CHOZI LA HERI

**JIBU SWALI LA 2 AU 3**

**2**. "Itakuwa kama kukivika kichwa cha kuku kilemba"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(ala 4)**

(b) Fafanua athari zinazotokana na kuvikwa kilemba kichwa cha kuku. **(ala 16)**

**3.** Eleza jinsi uozo unavyoshughulikiwa katika Riwaya ya Chozi la heri. **(ala 20)**

## TAMTHILIA YA KIGOGO

**JIBU SWALI LA 4 AU 5**

4. "Uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mpenzi.

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(ala 4)**

**(b)** Eleza mbinu mbili za lugha katika dondoo hili. **(ala 4)**

**(c)** Taja hulka mbili za mnenaji katika dondoo hili. **(ala 2)**

**(d)** Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii huku ukirejelea tamthilia ya Kigogo. **(ala 10)**

**5.** Viongozi katika nchi zinazoendelea wamejawa na tamaa.
Thibitisha kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya Kigogo. **(ala 20)**

## TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE

**JIBU SWALI LA 6 AU 7**

6. "Ndugu yangu kula kunatumaliza"
"kunatumaliza au tunakumalizia"

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(ala 4)**

**(b)** Fafanua maana ya kitamathali katika kauli "kula tunakumaliza"
Kwa kurejelea hadithi "shibe inatumaliza" **(ala 10)**

**(c)** Kwa mujibu wa hadithi hii kula kunawamaliza vipi. **(ala 6)**

**7.** (a) Ubahaimu unaotendewa mwanamke una athari mbaya kwake. Fafanua kwa kutolea mifano huku ukirejelea hadithi ya "Mame Bakari" **(ala 10)**

(c) Mapenzi ni mateso, utumwa, ukandamizaji na ushabiki usio na maana.
Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi "Masharti ya kisasa" **(al 10)**

## FASIHI SIMULIZI

**8.** (a) Methali ni nini? **(ala 2)**

(b) Eleza sifa za methali. **(ala 6)**

(c) Andika methali zinazotumiia tamathali hizi. **(ala 4)**

(i) tashbihi
(ii) takrikri
(iii) tanakali za sauti
(iv) istiari

(d) Eleza umuhimu wa vitendawili katika jamii. **(ala 8)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 10 PAPER 1

**NAME………………………………………………… INDEX NO…………………**

**SCHOOL……………………………………… SIGN…………………………**

**DATE……………………………………**

## MASWALI

**1) LAZIMA**

Wewe ni waziri wa usafiri nchini. Kumekuwepo na ajali nyingi za barabarani hivyo basi umealikwa na kituo cha runinga cha Mzalendo Kufafanua sababu za ajali hizi. Andika mahojiano yenu.

**2)** Ujenzi wa reli za kisasa nchini una manufaa mengi kuliko madhara. Jadili.

**3)** Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:
Usitukane wakunga na uzazi ungalipo.

**4)** Andika kisa kinachomalizika kwa maneno yafuatayo:
**…** Baba niliyemfahamu kwa picha pekee, hatimaye aliwasili nyumbani baada ya miaka ishirini. Nilimkumbatia huku machozi yakitudondoka sote.

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 10 PAPER 2

NAME…………………………………………………… INDEX NO…………………

SCHOOL………………………………………… SIGN…………………………

DATE………………………………………

1. **UFAHAMU :** (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.***

Nchi nyingi duniani zimetia sahihi mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki hizi ni pamoja na uhai, lishe bora inayotosha na makazi bora yaliyo salama. Hali kadhalika, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu inastahili kutolewa bure, iwe inafaa na inayopatikana kwa urahisi. Isitoshe , mtoto hastahili kupigwa, kudunishwa, wala kubaguliwa kwa namna yoyote ile: iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vinginevyo.Mtoto hapaswi kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kushurutishwa. Vile vile , mtoto anastahili kushirikishwa katika kufanya maamuzi yanayoweza kumwathiri maishani. Pia mtoto ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalum na habari kuhusu masuala mbalimbali. Pamoja na hayo anastahili kupendwa na kuheshimiwa kimawazo na kihisia.

Haki za watoto zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, serikali na wazazi wakiwa katika mstari wa mbele. Hii ndiyo sababu serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba na sheria za nchi husika.Yeyote anayezikiuka anapasa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria .Walakini , haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Kuna watoto ambao hawajawahi hata kupata kibanda cha kuweka ubavu. Wengi wa hawa wamejipata wakiselela kwenye mitaa na hata majaa ya mji na vijiji ambako hulazimika kupitisha usiku hata katika majira ya kipupwe na masika! Wengine hawapati chakula: licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi: kwani hata awamu moja ni adimu kupata! La kusitikisha ni kwamba wale wanaotarajiwa kuwa **vigogo** wa kuzilinda haki hizi ndio wanaoongoza katika kupalilia ukiukaji wazo. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kushinikizwa kufanya kazi za sulubu kipunda, kunyanyaswa kinjinsia, kuishi katika

mazingira hatari na hata kuuawa. Baadhi ya wanaohusika na vitendo hivi hasi huwa wazazi au jamaa wa karibu kama vile mjomba, shangazi au wahudumu wa nyumbani.

Madhila yanayowapata watoto hayatokei tu katika mazingira ya nyumbani. Mateso huvuka mipaka na kufikia ngazi ya kimataifa. Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Linalokata maini ni kwamba baadhi ya viongozi katika mataifa haya hawafanyi lolote kuwanusuru. Lao huwa kuwatazama watoto wanaotakiwa kuwalinda wakigeuzwa kuwa mababe wa kuua na kuuana.Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia hulazimika kuvaa mabuti ya kijeshi ambayo **huwa nanga kwao** kubeba, licha ya bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani.

Mojawapo ya mambo ambayo viongozi nchini humu walilenga shabaha kuyafikia baada ya kijinyakulia uhuru ni elimu kwa wote. Hata hivyo, hii imekuwa kama ndoto isiyotabirika katika baadhi ya janibu. Ni kweli kwamba sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi nchini humu inaendelea kutekelezwa. Hata hivyo, asilimia ya watoto na hata watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ingali kubwa. Jukwaa la vijiji nchini humu na hata katika mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu limesheheni idadi kubwa ya watoto wasioenda shuleni. Kichocheo kikuu cha hali hii ni kwamba wazazi na walezi wamejipata katika lindi la ufukara uliokithiri. Hata wanapojitahidi kujinyanyua na **kujikuna wapatapo** kuyakidhi mahitaji ya kielimu ya wanao, wao hujipata wakitapatapa katika kinamasi hicho hicho cha ulitima. Matokeo ni kwamba watoto wa matajiri wanaendelea kuelimika huku wa maskini wakibakia kwenye kiza cha ujinga. **Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kama kwamba ni waota ndoto za mchana.**

Hali ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe ttufanye hima tuungane mikono na kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu utekelezaji wa haki za watoto. Twapaswa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma , mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati.

## MASWALI

**(a)** Huku ukitoa mifano **minne**, eleza hali ya kinyume inayojitokeza katika aya ya pili. **(alama 4)**

**(b)** Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu. **(alama 3)**

**(c)** Kwa kurejelea aya ya nne , onyesha mchango wa serikali katika kuwajibikia haki za watoto**.** **(alama 3)**

**(d)** "Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu. **(alama 2)**

**(e)** Eleza maana ya msamiati ufuatayo kama ulivyotumika katika taarifa. **(alama 3)**

**(i)** Vigogo…………………………………………………………………………

**(ii)** Huwa nanga kwao……………………………………………………

**(iii)** Kujikuna wajipatapo……………………………………………

## 2. MUHTASARI (Alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwa uchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea wenzo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema ‘maarifa ni nguvu.’

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha,kuyatawala na kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ambaye ameyakosa maarifa Fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huadhirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanaweza kuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwana methali ya Kiswahili: ‘Elimu ni mali.’ Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upizani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watuwengine wengi pasiwe na upizani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa.kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha maarifa mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu mmoja huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu hawezi kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo mzito wa maarifa kichwani

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo Fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishwa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele Fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambamba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa

muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana. Kwa mfano , neno ‘mwerevu ‘huweza kuwa na maana kwa kuweka katika muktadha wa ‘mjinga’, ‘mjanja’, ‘hodari’, na kadhalika.

Maarifa huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknologia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu, ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kianachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kudhibitiwa au kuzuiliwa mahali Fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapo mfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe, ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia Fulani za ueneaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

## MASWALI

***(a)*** Fupisha aya ya pili na ya tatu. (maneno 55-60) (*alama 5, 1 ya utiririko)*

**Matayarisho**

Nakala safi

**(b)** Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane. (maneno 100-110) (alama 10, 2 za utirriko)

Matayarisho

**Nakala safi**

## 3. MATUMIZI YA LUGHA **(ALAMA 40)**

**(a)** Tofautisha sauti zifuatazo. **(alama 2)**

(i) /t/ /s/

(ii) /h/ /gh/

(iii) /o/ /u/

(iv) /b/ /a/

**(b)** (i) Mzizi ni nini**?** **(alama 1)**

(ii) Toa mfano wa kitenzi chenye mzizi huru**.** **(alama 1)**

**(c)** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama 2)**

N+RH+t+E

**(d)** Ainisha mofimu katika neno lifuatalo: **(alama 2)**

Kiokoteni

**(e)** Andika katika ukubwa**.** **(alama 1)**

Paka hawa wamemfukuza mbwa wetu.

**(f)** Taja matumizi mawili ya kiambishi /e/ **(alama2)**

**(g)** Andika upya ukifuata maagizo**.** **(alama 3)**

**(i)** Maji ambayo wanakunywa ni hatari. (Andika katika hali ya mazoea bila kutumia amba)

**(ii)** Watu wengi walihasirika bomu lilipolipuka katika jengo hilo. (Tumia nomino badala ya vitenzi vilivyopigwa mstari.)

**(iii)** Pombe hiyo ilimfanya kuwa kipofu. (Tumia kitenzi badala ya neno lililopigiwa mstari)

**(h)** Tunga sentensi ukitumia kishazi tegemezi kinachofanya kazi ya kielezi. **(alama 2)**

**(i)** Bainisha aina ya vitenzi katika sentensi ifuatayo. **(alama 3)**

Wao si wahalifu ingawa walikuwa msituni walipokamatwa.

**(j)** Tunga sentensi ukitumia nomino waya pamoja na kivumishi cha pekee cha kusisitiza. **(alama 2)**

**(k)** Andika katika usemi halisi. **(alama 2)**

Hamisi alimwambia nyanya yake kuwa siku hiyo hakuwa na nafasi lakini angemtembelea siku ambayo ingefuata.

**(l)** Changanua kwa jedwali. **(alama 2)**

Mwenye njaa hana miiko.

**(m)** Taja matumizi mawili ya parandesi. **(alama 2)**

**(n)** Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu / dhamira yake. **(alama 1)**

Rais amepiga marufuku ukataji miti nchini.

**(o)** Andika katika umoja. **(alama1)**

Hao wameharibu nyua zilizotengenezwa kwa mbao.

**(p)** Andika katika wakati uliopita hali timilifu **(alama 1)**

Miti katika msitu huo inakauka.

**(q)** Andika upya ukitumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. **(alama 2)**

Nyanya alisomba taka na kuitia katika jaa lililo shambani.

**(r)** Huku ukitoa mifano mwafaka taja miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U/I **(alama 2)**

**(s)** Tunga sentensi ukitumia **na** kama: **(alama 2)**

(i) Kihusishi

(ii) Kuonyesha umilikaji

**(t)** Onyesha kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. **(alama 3)**

Polisi ambao walikuja juzi waliwakamata majambazi wote jana jioni.

**(u)** Tunga sentensi mbili kuonyesha maana mbili za neno **muhali.** **(alama 2)**

**(v)** Andika methali inayoafiki maelezo yafuatayo .

Ni afadhali kupata matatizo madogo kwa sasa ili kuyaepuka mengi baadaye.

## ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyodhibiti mitindo ya lugha

(i) Mazingira **(alama 2)**

(ii) Mada **(alama 3)**

**(iii)** Hali **(alama 2)**

(b) Fafanua sera tatu ambazo zimepitishwa na serikali zinazochangia kuimarika kwa lugha ya Kiswahili**.** **(alama 3)**

# KCSE FINAL PREDICTION

# KISWAHILI

## TRIAL 10 PAPER 3

NAME………………………………………………… INDEX NO…………………

SCHOOL………………………………………… SIGN………………………

DATE………………………………………

## SEHEMU YA A: HADITHI FUPI

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda; Tumbo lisiloshiba na hadithi nyingine.**

1. **Lazima**

"Usiteketeze umati kama kuni zinavyoteketeza moto. Rudi, rudi kwa Mola wako."

**a.** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(ala 4)**

**b.** Eleza tamathali mbili za usemi zinavyojitokeza katika dondoo hili **(ala 2)**

**c.** Eleza madhara yanayotokana na vitendo vya mnenewa vya kuteketeza umma. **(ala 8)**

**d.** Eleza umuhimu wa mnenaji wa maneno haya. **(ala 6)**

## SEHEMU YA B: TAMTHLIA

**PAULINE KEA: KIGOGO**

Jibu swali la 2 au 3

2. "Hata nami naona pengine amenusa sumu."

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(ala 4)**

**b)** Eleza ni kwa nini mrejelewa anasemekana kuwa amenusa sumu. **(ala 2)**

**c)** Tambua mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. **(ala 1)**

**d)** Mwandishi wa Tamthlia hii amefaulu sana katika matumizi ya mbinu hii uliyotaja hapo juu. Kwa kutoa hoja saba thibitisha haya. **(ala 7)**

**e)** Eleza umuhimu wa mzungumziwa **(ala 6)**

3. "Fungua macho uone. Keki imeliwa kwingine, mwaletewa masazo.

**i)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(ala 4)**

**ii)** Tambua mbinu ya kisanaa iliyotumika katika dondoo **hili** **(ala 4)**

**iii)** Thibitisha kuwa keki imeliwa kwingine **(ala 6)**

**iv)** Eleza sifa za msemaji wa maneno haya **(ala 6)**

## SEHEMU YA C: RIWAYA YA CHOZI LA HERI

**ASSUMPTA K. MATEI.**

Jibu swali na 4 au 5

**4.** "Vipi binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?

**a.** Eleza muktadha wa dondoo hili **(ala 4)**

**b.** Tambua mbinu ya lugha iliyotumika **(ala 2)**

**c.** Jadili sifa tatu za msemaji **(ala 3)**

**d.** Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika Riwaya **(ala 11)**

**5.** " Kiu ilipobisha hodi, tulijaribu kujikuna tulipojipata."

**A)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(ala 4 )**

**B)** Tambua tamathali mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. **(ala 4)**

**C)** Kando na tatizo lililodokezwa katika dondoo hili, eleza matatizo mengine sita waliyokumbana nayo msemaji na wenzake. **(ala 6)**

**D)** Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya **(ala 6)**

## SEHEMU YA: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7*

*6.* ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

**SIPENDI KUCHEKA**

Pana jambo natukiya, kwangu hilo muhali,
Kitenda naona haya, kujishusha yangu hali
Sipendi unipe hidaya, sipendi kutenda hili
Sipendi mimi kucheka

Sipendi mimi kucheka, kuchekea mawi
Sipendi na ya dhihaka, kwangu nyemi hiwi
Sipendi kwa hakika, mwovu kistawika
Halafuye nikacheka!

Maskini akiteswa
Yatima akinyanyaswa
Mnyonge naye akinyonywa
Sipendi hata ikiwa
Uwezo nguvu najuwa
Ni hili sitatekezwa

Mbona lakini nicheke, kwayo furaha?
Na wewe ukajiweke, uli na siha?
Na yatima ali pweke, ye anahaha?
Amenyimwa haki yake, hanayo raha!
Na moyo wangu ucheke, kwa ha ha, ha!
Kumbuka kwa kucheka Mimi katu sitacheka.

## Maswali

**a)** Shairi hili ni la aina gani? Thibitisha **(ala3)**
**b)** Taja sababu zinazomfanya mshairi asitake kucheka. **(ala3)**
**c)** Chambua umbo la shairi hili kwa kuzingatia ubeti wa mwisho. **(ala4)**
**d)** Tambua nafsineni na nafsinenewa katika shairi hili. **(al2)**
**e)** Tambua toni ya shairi hili. **(ala1)**
**f)** Fafanua uhuru wa mshairi katika shairi hili. **(ala2)**
**g)** Andika ubeti wa pili kwa lugha tutumbi. **(ala3)**
**h)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumka katika **shairi** **(ala2)**
(i) Mawi
(ii) Nyemi

*7.* ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yatakayofuata.***

Kimya changu kimezidi, navunja yangu subira,
Narejeya miradi, kuhitimisha dhamira,
Kukejeli sina budi, niwafunze utu bora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Serikali bila hadi, ndo kiini cha madhara,
Yanopiga kama radi, isokuwa na ishara,
Yamini kuwa gaidi, watupora mishahara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Wamejifanya hasidi, wasopatana fikira,
Wana yao makusudi, kujisombea ujira,
Wakilenga kufaidi, tumbo zao za kichura,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Nchi yetu kufisidi, ni jambo linonikera,
Tangia siku za jadi, ufukara ndo king'ora,

Kutujazeni ahadi, nyie mkitia fora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Fakiri watozwa kodi, wa pwani na walo bara,
Kwa uvumba hata udi, mwawalipa kwa hasara,
Hamudhamini miradi, mejihisi masogora,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Mesema kazi ni chudi, basi sirikali gura,
Nafsi zenu mzirudi, mkubali kuchakura,
Makondeni mkirudi, muondoe ufukara,
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

Ujanjenu umezidi, demokrasia bakora,
Debeni takaporudi, michirizi kwenye sura,
Kuwachuja ndo! muradi, kwa za mkizi hasira
Nani aali zaidi, Wakenya au vinara?

***<u>Maswali.</u>***

**a)** Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. **(ala1)**
**b)** Ainisha shairi hili kwa jinsi tatu huku ukitoa sababu. **(ala3)**
**c)** Onyesha mbinu mbili za lugha katika shairi hili. **(ala2)**
**d)** Bainisha matumizi matatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. **(ala3)**
**e)** Andika ubeti wa nne katika mtindo tutumbi. **(ala4)**
**f)** Fafanua maudhui matatu yanayojitkeza katika shairi hili. **(ala3)**
**g)** Taja mpango mmoja unaotajwa kama njia ya kutatua matatizo ya nchi. **(ala1)**
**h)** Eleza muundo wa shairi hili. **(ala3)**

## <u>SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI</u>

**8. (a)** Eleza sifa tatu za nyimbo. **(ala6)**

**(b)** Tofautisha dhana zifuatazo: **(ala4)**

III) Misimu na misemo
IV) Ulumbi na malumbano ya utani.

**(c)** (i) Eleza maana ya mawaidha. **(ala2)**

(ii) Fafanua majukumu manne ya mawaidha katika jamii. **(ala8)**

# THE END

## THIS IS THE 1st SERIES OF FINAL KCSE PREDICTION KISWAHILI EXAMINATIONS TRIALS

## A SET OF POSSIBLE KCSE QUESTIONS

# CALL/TEXT/WHATSAPP

# 0746 222 000

*mwalimuagency@gmail.com*

# TO ALL KCSE CANDIDATES;

## SUCCESS IN YOUR KCSE EXAMS.

## BY; MWALIMU AGENCY TEAM.

# FOR THE FOLLOWING;

## PRIMARY SCHOOL EXAMS

- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SERBOOKS GUIDE BOOKS
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ LESSON PLANS
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ CROSSCOUNTRY PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ CROSSCOUNTRY MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ CROSSCOUNTRY PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS
- ✓ MWALIMU MOCKS SERIES
- ✓ NATIONAL SCHOOLS MOCKS
- ✓ SUBJECTS JOINT MOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ CBC RESOURCES
- ✓ KASNEB RESOURCES

- ✓ COLLEGE MATERIALS
- ✓ UNIVERSITY EXAMS

# CAUTION TO KCSE CANDIDATES:

**IN THE EVENT YOU REALIZE PART/ALL OF THESE QUESTIONS WERE DIRECTLY OR INDIRECTLY LIFTED IN THE FINAL KCSE EXAMS, PLEASE, DO NOT PANIC!**

**KILA LA HERI**

***SUCCESS***